Nipashe
MWANGA WA JAMII
Jumapili Desemba 8, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • No. 0581884
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US
JUMAPILI
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital
epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com
MIAKA 30 Nipashe
Mwanga wa Jamii
www.ippmedia.com

# Kanisa lashtushwa kasi ya mauaji

• **Lasema** ni chanzo cha laana katika ardhi, jamii ijitafakari... *Endelea ukurasa 2*

UKURASA WA 3

**WABUNGE WANNE WA AJALI YA BASI WARUHUSIWA**

UKURASA WA 3

**TRC YAONGEZA SAFARI MIKOA YA KASKAZINI MSIMU SIKUKUU**

UKURASA WA 3

**MIRADI YA UCHUMI YACHOCHEA Z'BAR KUSAKA UMEME WA UHAKIKA**




UKURASA WA 22

**PSG HAINA MPANGO NA MO SALAH**

RAIS wa klabu ya PSG, Nasser Al-Khelaifi amesema...

## Wanne mbaroni tuhuma mauaji mtumishi TRA

UKURASA 2



Dereva wa pikipiki maarufu bodaboda, akiwa amebeba wanafunzi wanne, mtindo maarufu kama mshikaki, kitendo ambacho ni hatari kwa usalama barabarani. **PICHA: MTANDAO**

RIPOTI MAALUM

## Hatari watoto kubebwa wanne kwenye bodaboda

UK. 4

**MICHEZO** SIMBA KAMILI KUIVAA CS CONSTANTINE UK.24 **KATUNI** UK.6

# Wanne mbaroni tuhuma mauaji mtumishi TRA

**Na Romana Mallya**

SIKU mbili baada ya watumishi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), kujeruhiwa kwa kipigo kutoka kwa wananchi na mmoja kuripotiwa kufariki dunia, Jeshi la Polisi Kanda Maalum Dar es Salaam, limetangaza kuwashikilia watu wanne kwa tuhuma za mauaji.

Kamanda wa Polisi wa Kanda hiyo, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Jumanne Muliro, aliwataja wanaowashikilia ni Deogratius Massawe (49) na Iddi Bakari (30), wote wakazi wa Tegeta kwa Ndevu, wote makuli.

Wengine aliwataja ni Omar Issa (47) ambaye ni mpiga debe wa bodaboda, mkazi wa Bunju, Kinondoni, Dar es Salaam na Rashid Mtonga, (29) dereva wa bodaboda mkazi wa Bunju, Dar es Salaam.

Kamanda Muliro alisema wanatuhumiwa kufanya mauaji ya mtumishi TRA, Amani Simbayao na kumjeruhi Adriano Fredrick.

"Watuhumiwa hao na wengine ambao bado wanahojiwa kwa kina, walikamatwa baada ya kuwashambulia maofisa hao wa TRA wakati wakitekeleza majukumu yao ya kisheria.

"Waliliharibu pia, gari namba STL 9923 aina ya Toyota Land Cruiser Hardtop jeupe mali ya TRA. Tukio lilitokea Desemba 5, mwaka huu, saa 3 :00 usiku, Tegeta kwa Ndevu, Kinondoni, baada ya maofisa hao wa TRA kukamata gari namba T 529 DHZ aina ya BMW rangi nyeupe lililodaiwa kuwa na makosa ya kikodi," alisema.

Kamanda Muliro alisema Jeshi la Polisi linaonya vikali na kwamba halitavumilia watu ambao wanataka kujenga tabia ya kuwashambulia watumishi wa serikali wakati wakitekeleza majukumu yao, licha ya kuwa wanakuwa wamefuata taratibu zote za kisheria.

Alisema jeshi halitasita kuchukua hatua kali za haraka na za kisheria dhidi ya wahusika kwa kuwafikisha kwenye mamlaka zingine za haki.

Taarifa iliyotolewa juzi usiku na TRA, ilitangazia umma kwamba mfanyakazi wake, Simbayao, amefariki dunia juzi mchana akiendelea na matibabu katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH).

"Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na Watumishi wa TRA inasikitika na kutoa pole kwa familia, ndugu na jamaa, kutokana na kifo cha mtumishi wetu wa TRA Amani Simbayao.

"Kifo hicho kilitokea juzi (Desemba 6) mchana Hospitali ya Muhimbili alikolazwa baada ya tukio la shambulio akiwa katika majukumu yake ya kiazi kwa maslahi ya taifa eneo la Tegeta kwa Ndevu," ilisema taarifa hiyo.

Watumishi hao wanadaiwa kushambuliwa na wananchi wakati wanatimiza wajibu wao wakihusishwa na kitendo cha utekaji, kilichosababisha wao na gari kushambuliwa.

Gari lililokuwa likifuatiliwa ni namba T 229 DHZ aina ya BMW X6 linalodaiwa kuingizwa nchini kinyume bila kulipa kodi za serikali stahiki kwa mujibu wa sheria, hivyo watumishi hao walikuwa wakiifuatilia kwa lengo la kuikamata, ili kuchukua hatua stahiki kwa mujibu wa sheria za kodi.

*Kwa maoni: +255 677 020 701*
*Email: customerrelations@guardian.co.tz*



Wakazi wa Monduli Juu, wilayani Monduli, mkoani Arusha, wakipata elimu kuhusu uboreshaji Daftari la kudumu la Mpiga Kura kutoka katika gari la Elimu ya Mpiga Kura la Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC), wilayani humo, jana. Uboreshaji wa daftari hilo kwa mikoa ya Arusha, Kilimanjaro na baadhi ya Halmashauri za Chemba, Kondoa na Kondoa mji, mkoani Dodoma, unatarajia kuanza Disemba 11 hadi 17 mwaka huu. **PICHA: INEC**

# Kanisa lashtushwa na kasi ya mauaji

**Na Mary Mosha,** MOSHI

PAROKO wa Parokia Teule ya Kifuni, Padri Timoth Tingo, amesema mauaji yamekuwa tatizo Tanzania, hivyo kuna haja ya jamii kujitafakari kwa sababu husababisha laana katika ardhi.

Alisema hayo jana katika ibada ya maziko ya Isaack Mallya, ambaye ni kaka wa Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Kilimanjaro, Patrick Boisafi, aliyeuawa kikatili kwa kucharangwa mapanga kichwani na shingoni baada ya kuvamiwa nyumbani na watu wasiojulikana.

"Kila siku ukifungua vyombo vya habari hapa nchini utakutana na mauaji. Mume kumuua mke, mke kamuua mume, watoto kuua wazazi, jirani kuuawa. Hii yote ni kutokana na chuki, hasira na kutaka kulipiza kisasi," alisema.

Desemba 2, mwaka huu, majira ya asubuhi, watu wasiojulikana walivamia nyumbani kwa Mallya wakati akijiandaa kwenda ibada ya misa takatifu katika Kijiji cha Umbwe Onana, Kata ya Kibosho Magharibi, mkoani Kilimanjaro na kumpiga maeneo mbalimbali ya mwili ikiwamo kichwani.

Kutokana na hali hiyo, alisema kuna haja ya jamii kujitafakari kwa sababu mauaji hayo huleta laana katika ardhi na hivyo kuleta madhara makubwa kwenye vizazi vyao.

"Kila mmoja aliyefika hapa (kwenye maziko) ajitafakari amekuwa muuaji mara ngapi kwa kulipiza kisasi, kujenga chuki, hasira, kutamka maneno ya uongo na matamshi ya kuuwa kwa watu wetu wa karibu.

"Kuhusu tukio hili, polisi tunaamini mtatenda haki na ninyi mtoe ushirikiano ili haki itendeke lakini niwasisitize tutoe ushirikiano. Tuache kutaka fedha za haraka bila kufanya kazi, "alisema Padri Tingo.

Aliwataka vijana kupenda kufanya kazi na kuridhika na wanachopata na kuhakikisha wanakuwa na nidhamu ili kuleta mabadiliko katika maisha yao.

"Vijana fanyeni kazi. Akili isiyofanya kazi ni karakana ya shetani. Pendaneni, heshimianeni, msitafutane tu kwa vikao vya send off (sherehe ya kumuaga binti anayeolewa), harusi, msiba na sherehe. Badala yake itaneni msaidiane, onyaneni, saidianeni na hakikisha mnaleta mabadiliko ya kifikra,

"Na nyinyi wanandoa, hakikisheni ndoa zetu zinakuwa mifereji ya kwenda mbinguni. Acheni kutukanana na kutishiana kila siku nitakuuwa, Hebu waombeeni baraka," alisema.

Akitoa salama za pole kwa familia, mwanaharakati Vick Massawe, alitaka viongozi wa serikali kuchukua hatua hasa kwa baadhi ya vijana wanaofanya uhalifu na wanaotumia dawa za kulevya aina ya bangi, pombe kupitiliza walioko katika Kata ya Kibosho Magharibi.

"Katika kata hii, bangi inauzwa kama njugu. Ukienda kuripoti polisi kabla hajafika tayari mtuhumiwa kashafika hali inayofanya watu kutishwa ndiyo maana ndani ya nyumba yake mmekuta RB nyingi kwani alikuwa anatoa taarifa kila wakati.

"Katika kata hii, hiki ni kifo cha 12 kwa muda mfupi tu. Polisi mtusaidie kupata haki na matukio haya yageuke kuwa historia,"alisema.

Katibu Tawala Mkoa Kilimanjaro, Kiseo Nzowa, alilitaka Jeshi la Polisi kuhakikisha watuhumiwa wanakamatwa na kuwaomba wananchi kutoa taarifa ili zisaidie upatikanaji wa haki.

"Wananchi ni lazima tutunze amani, tutoe taarifa tunajua kuwa mnawajua na mnaishi nao, na tujue kuwa kutoa taarifa ni kumaliza tatizo.

"Haya mambo ya mauaji tusiyaone ya kawaida hata kidogo, tujiepushe na migogoro, chuki, na visasi haviwezi kutusaidia chochote katika maisha yetu, na tutambue tusipotoa ushirikiano kesho litakuja kwako, hawa ni vijana wetu wanaotekeleza matukio hayo," alisema.

Kamanda wa Polisi Mkoa Kilimanjaro, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Simon Maigwa, alisema tayari wamewakamata watu wanne kuhusiana na tukio hilo na kuitaka jamii kama ina taarifa yoyote ya ziada iwasilishwe kituoni.

"Tangu tulipopata taarifa hizi, tumefanya msako mkali na tumewakamata watu wanne na tunaendelea kwa uchunguzi, tunawaomba yeyote mwenye taarifa ya ziada asisite kuitoa.

"Ila jamiii tunaomba ushirikiano wenu. Vijana hawa ni wetu na hapa nimesikia kuwa huyu ni mtu 12 kuuawa, sijui ni kabla sijaja au la. Ila ninaomba vyombo vyangu tutayafanyia kazi, haki itapatikana, niwahakikishia mkoa uko salama sana,"alisema Kamanda Maigwa.

*Kwa maoni: +255 677 020 701*
*Email: customerrelations@guardian.co.tz*

# TRC yaongeza safari za treni mikoa ya kaskazini

**Na Grace Mwakalinga**

SHIRIKA la Reli Tanzania (TRC), limetangaza ongezeko la safari za treni kwenda mikoa ya Tanga, Kilimanjaro, na Arusha katika kipindi cha sikukuu za mwisho wa mwaka.

Kwa miaka mingi, wakati wa msimu wa sikukuu za Krismasi na Mwaka Mpya, kumekuwa na mahitaji makubwa ya usafiri kwa mikoa hiyo. Kutokana na hali hiyo, TRC kwa miaka ya karibuni imekuwa ikiongeza safari za treni kwa abiria wanaokwenda na kutoka katika mikoa hiyo.

Kwa mantiki hiyo, TRC imesema hatua hiyo inalenga kukidhi mahitaji ya usafiri kwa abiria wengi wanaosafiri kuelekea Kaskazini Mashariki mwa Tanzania.

Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano wa TRC, Fredy Mwanjala, katika taarifa yake jana, alisema safari mpya ya treni itaongezwa siku ya Jumatano, hivyo kufanya jumla ya safari tatu kwa wiki kwenda na kutoka katika mikoa hiyo.

"Kuanzia Jumatatu mpaka mwanzoni mwa Januari 2025, treni zitakuwa zikibeba mabehewa 18 kwa safari moja, zenye uwezo wa kubeba abiria kati ya 1,000 na 1,200 kwa wakati mmoja," alisema Mwanjala.

Alisema licha ya ongezeko la safari hizo, TRC haitakuwa na ongezeko la nauli katika kipindi hiki cha sikukuu, bali zitasalia kama zilivyo sasa.

"Safari za Moshi, nauli zitakuwa Sh. 16,500 kwa daraja la tatu, 23,000 kwa daraja la pili kukaa na 39,000 kwa daraja la pili kulala. Vilevile, kwa safari za Arusha, nauli zitakuwa Sh. 18,700 kwa daraja la tatu, Sh. 26,700 kwa daraja la pili kukaa na Sh. 44,400 kwa daraja la pili kulala," alisema Mwanjala.

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations @guardian.co.tz***

# Wabunge waliopata ajali majina yatajwa, wanne waruhusiwa

**Agusta Njoji na Renatha Msungu,** DODOMA

WABUNGE wanne kati ya 17 waliolazwa katika Hospitali ya Benjamini Mkapa (BMH) wameruhusiwa, huku majina yao yakitajwa.

Majeruhi hao walipata ajali juzi eneo la Mbande wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma wakienda Mombasa, Kenya kwenye mashindano ya 14 ya Mabunge ya Afrika Mashariki.

Kamanda wa Polisi mkoani humo, George Katabazi, jana alitaja majina ya wabunge waliojeruhiwa kuwa ni, Mbunge wa Nkenge (CCM), Florent Kyombo, Mbunge wa Viti maalum (CCM), Asia Halamga, Mbunge wa Mbogwe (CCM), Nicodemas Maganga, Mbunge wa Viti maalum (Chadema), Grace Tendega, Mbunge wa Viti maalum (CCM), Suma Fyandomo.

Wengine aliwataja ni Mbunge wa Viti maalum (CCM), Zulfa Mmaka Omar, Mbunge wa Igunga (CCM), Nicholaus Ngassa, Mbunge wa Viti maalum (CCM), Juliana Shonza, Mbunge wa Viti maalum (CCM), Catherine Magige na Mbunge wa Mtwara Vijijini (CUF), Shamsia Mtamba.

Mbunge wa Amani (CCM), Abdul Yussuf Maalim, Mbunge wa Iringa Mjini (CCM), Jesca Msambatavangu, Mbunge wa Hai (CCM), Saashisha Mafuwe, Mbunge wa Vitimaalum (CCM), Furaha Butondo, Mbunge wa Magomeni (CCM), Mwanakhamis Kassim Saidi, Mbunge wa Wingwi (CCM), Omar Issa Kombo na Mbunge wa Tabora Mjini (CCM) Emanuel Mwakasaka.

Akizungumza na Nipashe jana, Mkuu wa Idara ya Magonjwa ya Dharura wa BMH, Dk. Winnie Msangi, alisema kati ya wabunge hao, wanne wameruhusiwa baada ya kufanyiwa uchunguzi na madaktari bingwa hospitalini hapo na afya zao kuonekana kuimarika.

Dk. Msangi alisema majeruhi wengine waliosalia wanaendelea kupatiwa matibabu chini ya uangalizi wa madaktari, ili kuhakikisha afya zao zinaimarika na kuendelea na shughuli zao za kila siku.

Ajali hiyo ilitokea juzi na kusababisha majeruhi 23 ambao walipelekwa katika mospitali mbalimbali ikiwamo BMH kwa ajili ya kupatiwa matibabu.

Kwa mujibu wa Kamanda Katabazi juzi, ajali hiyo ilitokea saa 2:00 asubuhi katika barabara kuu ya Dodoma- Morogoro eneo la Mbande, Kongwa na kusababisha majeruhi ambao ni wabunge 17, askari wawili, maofisa wa bunge wawili, dereva na kondakta.

Katabazi alisema chanzo cha ajali hiyo ni uzembe wa dereva aliyekuwa anaendesha basi la kampuni ya Shabiby, kushindwa kuchukua tahadhari wakati akitaka kulipisha gari lililokuwa mbele yake alilotaka kulipita.

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations @ guardian.co.tz***



Mdau Maendeleo Jimbo la Vunjo, mkoani Kilimanjaro, Enock Koola akiwaongoza wananchi katika zoezi la upandaji miti, shule ya seminari Agape, kata ya Mamba Kusini, wilayani Moshi jana, kuelekea sherehe za maadhimisho ya miaka 63 ya Uhuru wa Tanganyika. **PICHA: ASHRACK MIRAJI**

# Miradi Uchumi yachochea Zanzibar kusaka umeme

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema Zanzibar inadhamiria kuwa na umeme wa uhakika kutokana na kupanuka kwa shughuli za uchumi, miradi mikubwa ya maendeleo, ongezeko la hoteli za kitalii na kasi ya uwekezaji inayokua kila siku.

Dk. Mwinyi ameyasema hayo Ikulu, Zanzibar, wakati akizungumza na ujumbe kutoka Kamisheni ya Umoja wa Ulaya ukiongozwa na Rita Laraujinha, Mkurugenzi Mwendeshaji wa Masuala ya Nje, Kanda ya Afrika baada ya kumtembelea.

Taarifa ya Idara ya Mawasiliano Ikulum Zanzibar ilimkariri Rais Mwinyi akisema kwa muda mrefu Zanzibar imekuwa ikipokea megawati 100 za umeme kutoka Tanzania Bara kupitia waya za chini ya bahari ambao kwa sasa hautoshelezi.

Alisema kuna kila sababu ya kupata umeme mbadala na kufikiria kuwa na umeme wa jua, mawimbi au upepo na kuomba Umoja wa Ulaya (EU) kuangalia uwezekano wa kuisadia Zanzibar kwenye eneo hilo.

Dk. Mwinyi alisema serikali inafikiria kuzisarifu taka kwaajili ya kupata umeme mbadala, hatua ambayo itadhibiti taka zinazozalishwa kila siku.

Kuhusu uwezeshaji wanawake kiuchumi, Rais Mwinyi alisema nia ya serikali ni kuwaongezea nguvu, uwezo na utaalamu wakulima wa mwani ambao asilimia 90 ni wanawake.

Kadhalika alisema kuliinua zao hilo pamoja na kuanzisha viwanda vidogo na vya kati ili kuusarifu na kuzalisha bidhaa zinazotokana na zao hilo kwa kuziongezea thamani badala ya kuuza mwani kama malighafi.

Rais Mwinyi alisisitiza Umoja wa Ulaya kuiunga mkono Zanzibar katika azma yake ya kukuza uchumi kupitia sekta za kimkakati ikiwamo Uchumi wa Buluu na utalii ambazo ni sekta za kipaumbele kwa serikali anayoiongoza.

Alisema hivi sasa Zanzibar inafanya utalii wa kisasa unaoshajihisha utalii wa kumbi za mikutano, utalii michezo na wa afya, ambapo awali ilijikita zaidi kuendesha utalii wa fukwe na maeneo ya urithi, ambao umezoeleka kwa muda mrefu.

Rais Mwinyi azikaribisha nchi za Umoja wa Ulaya, hususan sekta binafsi kuja Zanzibar kubaini fursa za uwekezaji zilioko, kwani kuna maeneo mengi hayajafikiwa hasa kwa sekta ya Uchumi wa Buluu kupitia utalii, bandari, mafuta na gesi pamoja na sekta ya usafirishaji wa majini.

Kadhalika aligusia masuala ya jinsia na kueleza kuwa, serikali inafanya kila juhudi kuhakikisha inaweka uwiano sawa kwa wananwake na wanaume kwa nyanja zote.

Aliuomba Umoja wa Ulaya kuunga mkono kwenye maeneo ya taaluma, kuwajengea uwezo wanawake kwa dhamira ya kuwainua kiuchumi.

Wakati huo huo, Rais Mwinyi ameushukuru Umoja wa Ulaya kwa ushirikiano ulioko baina yao na misaada wanayoita kwa Tanzania husus Zanzibar kwa sekta za jamii hasa kwa elimu, afya na ustawi wa jamii na kuwaomba kuendeleza misaada hiyo.

Rita Laraujinha, ameipongeza Zanzibar kwa ushirikiano wanaoutoa kwenye miradi inayosimamiwa na EU na kumwakikishia Rais Mwinyi kuwa wataendelea kuiunga mkono Zanzibar wa kuleta maendeleo hasa kwa masuala ya afya, elimu na Uchumi wa Buluu. Alisema EU imerishwa na hali ya amani na utulivu ulioko Zanzibar na kwamba utaendelea wakati wote kuunga mkono juhudi za kuimarisha amani hiyo na kuona demokrasia inafuata mkondo wake kwaajili ya maendeleo ya nchi jamii kwa ujumla.

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations @ guardian.co.tz***

RIPOTI MAALUM

# Hatari watoto kubebwa wanne kwenye bodaboda

**Na Waandishi Wetu**

TAZAMA ulimwengu wanafunzi wanaobebwa kwenye bodaboda kwa mtindo wa mishikaki kuwahi shuleni. Huu ni utaratibu wa muda mrefu ambao sasa umechukuliwa kama wa kawaida, huku baadhi wakiishia kupata majeraha na wengine kuwa katika hatari ya kupoteza maisha.

Akiwa na miaka saba, mtoto wa Alex Simon, mkazi wa Mtaa wa Wigehe, Kata ya Zongomela, Kahama mkoani Shinyanga, wakati akirejea nyumbani akitoka shuleni, akiwa kwenye pikipiki aliunguzwa na bomba la kutolea moshi (exhaust).

Anasema licha ya mtoto huyo kupiga kelele kutokana na maumivu ya moto, dereva aliyembeba hakusikia kutokana na upepo mkali na kofia ngumu aliyokuwa amevaa hadi walipofika nyumbani.

"Nilitumia gharama kubwa kumtibu mtoto. Alikosa masomo kwa mwezi mzima. Binafsi siwezi kurudia tena kutumia usafiri huu wa pikipiki kumpakia mtoto wangu," anasema Simon.

Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani nchini, Naibu Kamishna wa Polisi (DCP) Ramadhan Ng'anzi, anasema licha ya kutokuwapo kwa ripoti za hivi karibuni zinazohusu matukio ya ajali za watoto wanaobebwa katika pikipiki, ni kosa kisheria kubeba abiria zaidi ya mmoja katika vyombo hivyo na pia, kumbeba mtoto mwenye umri chini ya miaka tisa.

**SHERIA**

Kanuni za usafirishaji kwa njia ya bajaji na pikipiki ya mwaka 2010 zilizofanyiwa marejeo mwaka 2017, zilizotungwa kupitia Sheria ya Utoaji Leseni za Usafirishaji ya Mwaka 2010, kanuni namba 14 (2) imepiga marufuku mtoto mwenye umri wa chini ya miaka tisa asibebwe kwenye pikipiki peke yake kama abiria.

Sheria ya Barabarani Kifungu cha 168 iliyofanyiwa marejeo mwaka 2002, kuhusu Sheria za Abiria anayetumia mabasi, daladala, teksi na pikipiki, imepiga marufuku kupanda pikipiki ambayo tayari imebeba abiria.

Kadhalika, imezuia mtoto mdogo kukaa mbele ya pikipiki au gari pamoja na mtu yeyote aliyebeba mtoto mdogo kukaa mbele.

Sheria hiyo pia imepiga marufuku kubeba zaidi ya abiria mmoja, ikishauri waendesha pikipiki au skuta pamoja na abiria wake, lazima wavae kofia ngumu iliyothibitishwa ambayo imefungwa kiusalama.

Pia imemtaka abiria wa kiti cha nyuma kukaa kwa kutanua miguu kwenye kiti halisi na kuweka miguu yote miwili kwenye sehemu ya kukanyagia.



Ukiukwaji wa sheria na kanuni hizo, mhusika anayekamatwa na kutiwa hatiani, atatozwa faini na kuzuiwa kuendesha na anaweza kupelekwa jela kwa miaka hadi mitano.

**WANANCHI**

Mmoja wa wananchi kutoka mikoa ya Kanda ya Ziwa, akiwamo mkazi wa Kata ya Nyasubi, Emmanuela Gwamagobe, anasema alfajiri na jioni wanafunzi hupakiwa kwenye pikipiki wakiwa wanne au zaidi.

Kutokana na hali hiyo, Gwamagobe anakishauri kitengo cha usalama barabarani kuwachukulia hatua madereva pikipiki wanaobeba wanafunzi kwa mtindo wa 'mishikaki' ambao huhatarisha maisha yao.

Anashauri wanaokutwa na makosa hayo walipishwe fani ya Sh. 30,000 badala ya Sh. 10,000 ya sasa na kuwabana wazazi ambao watoto wao wamepakiwa mtindo wa mishikaki kwenye bodaboda.

Mkazi wa Sengerema, mkoani Mwanza, Eugenia Lameck, anasema wakati mwingine watoto wanapakiwa kwenye vyombo hivyo, huku wanakokwenda ni karibu.

Mkazi wa Majengo, wilayani Magu, Godfrey Kweka, anasema kinachosababisha wazazi kuwapakia watoto wao kwenye pikipiki ni kurahisisha usafiri.

"Ukimwacha mtoto aende kupanda daladala analazimika kuamka saa 11 alfajiri na kufika shuleni saa tatu hadi saa nne asubuhi," anasema.

**KAULI ZA BODABODA**

Mwendesha bodaboda mkazi wa Mtaa wa Majengo, Magu, Jotham Kennedy, anasema sababu kubwa ya wazazi wanaowapa bodaboda watoto wao ili kuwapeleka shuleni na kuwarejesha nyumbani ni kutokana na kutokuwa na uwezo wa kugharamia magari ya shule na kukwepa usafiri wa umma kuepuka watoto wao kuchelewa shuleni.

Kennedy anasema kupitia kazi hiyo, wazazi wanawalipa kwa mwezi lengo likiwa ni kupunguza hatari ya mtoto kupotea kutokana na watoto wao kuwa wadogo.

Anasema huwalazimu kubeba watoto wengi katika pikipiki ili kuwasaidia kuongeza pato la mwisho wa mwezi.

"Ili kuingia makubaliano ni lazima awe anakufahamu vizuri. Mtoto mmoja kumpeleka na kumrudisha kwa kila siku ni Sh. 2,000 na kwa shule zilizoko karibu, wakiwa wawili ni sawa na Sh.4,000.

"Lakini mnaweza kufanya maelewano ukabeba Watoto wawili kwa Sh.3,000 kwa siku, hivyo unakuwa na uhakika wa Sh. 90,000 kwa mwezi. Ukiongeza watoto wengine wawili wa mzazi mwingine, inakuwa Sh. 180,000 hivyo inatusaidia kumaliza majukumu muhimu nyumbani," anasema Kennedy.

Anasema usafiri huo ni salama na unasaidia kumwepusha mtoto na vitendo vya ukatili njiani lakini tatizo lililoko ni kwa baadhi ya bodaboda kutokuzingatia sheria na usalama wa mtoto, hivyo kuhatarisha maisha yao kwa asilimia kubwa.

**CHANZO CHATAJWA**

Baadhi ya wazazi ambao watoto wao hubebwa katika pikipiki hizo, wanataja ugumu wa maisha kama chanzo cha wao kuruhusu watoto wao kubebwa katika usafiri huo wa pikipiki.

Mzazi na mkazi wa Sengerema, mkoani Mwanza, Peter Marco, anasema analazimika kuwapakiza watoto wake katika pikipiki moja kutokana na uwezo wa kifedha wa kumudu kuwalipia usafiri wa gari kuwa mdogo.

Anasema wazazi wamekuwa wakiungana ili Watoto wao wabebwe kwenye pikipiki moja kuepuka gharama.

Marco anasema kwa wastani kwa watoto wawili, hubebwa kwa gharama ya Sh. 3,000 (kwenda na kurudi nyumbani) kila siku.

Uchunguzi uliofanywa na Nipashe kupitia shule moja ya mchepuo wa Kiingereza mkoani Mwanza, imeonesha kwa miezi mitatu kwa mtoto anayetumia basi la shule ni Sh. 100,000 ambapo kwa usafiri wa pikipiki anachokwepa ni Sh. 10,000.

Fomu ya shule hiyo imebainisha kuwa kwa kila miezi mitatu mzazi atalipa fedha za usafiri Sh.100,000 na kuwa kwa vipindi vyote vine, mzazi atalipa Sh.400,000 ambako kwa wastani wa watoto wawili wanaobebwa katika pikipiki moja wanalipa Sh.3,000, sawa na Sh. 1500 kwa mtoto mmoja.

Kwa maana hiyo, mtoto anayetumia pikipiki kwa mwezi hutumia Sh. 30,000 na kwa miezi mitatu ni Sh. 90,000, tofauti ikiwa ni Sh.10,000 kulinganisha na mtoto anayetumia usafiri wa basi la shule.

Mzazi mwingine na mkazi wa Sengerema, Jenifer Christopher, maarufu kama Mama Petu, anasema anapoingia makubaliano na mtu wa pikipiki ili kumbeba mtoto wake, hafahamu kama mtu huyo ana makubaliano kama hayo sehemu nyingine.

"Shida ni kwamba, yule unayemwamini, kuna mzazi mwingine naye anamwamini, siwezi kumkatazamtu wa pikipiki kumbeba mtoto wa mwingine, ana haki ya kuwahi shuleni. Ninachowaomba bodaboda ni kuwa makini huko barabarani ili kuepusha ajali," anasema.

**WADAU WANENA**

Baadhi ya wadau wa elimu akiwamo, Diwani wa Kinamapula, Sharifu Samweli, anasema ubebaji wa abiria zaidi ya wawili katika pikipiki ni uvunjifu wa sheria za usalama barabarani.

Anasema wazazi wanaokodisha pikipiki ili kubeba watoto wao wanapokwenda shuleni na kurejea nyumbani hasa ni wale kutoka katika shule binafasi. Anasema katika kuondokana na tatizo hilo ni vema Jeshi la Polisi likashirikisha viongozi wa vyama vya waendesha pikipiki na bajaji kukabiliana ubebaji usiozingatia sheria.

Meneja wa Shule ya Sekondari Rwepa's, Frank Samweli, anakiri baadhi ya shule binafsi, wazazi wengi wamekuwa wakiwapeleka watoto wao kwa kutumia usafiri wa pikipiki na bajaji, wakiwa wamekaa zaidi ya wawili.

Samweli alishauri wazazi pamoja na madereva wanaochochea kuvunjwaji wa sheria za usalama barabarani, kuwajibishwa kisheria.

**KAULI YA POLISI**

Mkuu wa Kitengo cha Usalama Barabara Wilaya ya Kahama, Mrakibu Msaidizi (ASP) Flora Nangawe, anasema amefanya utafiti wake na kubaini wazazi na walezi wanaungana kukodisha pikipiki moja na kubeba watoto wao, jambo ambalo ni hatari.

Nangawe anasema wamejipanga kuchukua hatua za kisheria kwa dereva pikipiki atakayebainika amebeba wanafunzi kwa mtindo wa mishikaki, atatozwa faini ya Sh. 10,000 na makosa yanapojirudia atafutiwa leseni yake na mzazi atawajibishwa kisheria.

Askari wa usalama barabarani, Sajenti Mswadiku Kempantu, anasema mara kwa mara hutoa elimu kuhusu changamoto hiyo, lakini baadhi hukaidi na wanapokamatwa hutozwa faini na wakati mwingine hunyang'anywa pikipiki kwa muda ili wajirekebishe.

Mswadiku anasema pia, hairuhusiwi mtoto chini ya miaka tisa kubebwa na bodaboda kwa kukaa mbele kwenye tanki la mafuta.

**KANUNI YAJA**

DCP Ng'anzi, akizungumza na Nipashe, anasema licha ya kutokuwa na ripoti za hivi karibuni zinazohusu matukio ya ajali za watoto, lakini anakiri hilo ni kosa kisheria.

Anabainisha kwamba ni kosa si kwa dereva wa pikipiki kubeba abiria zaidi ya mmoja na pia kubeba mtoto mwenye umri wa chini ya miaka tisa katika vyombo hivyo.

Anasema operesheni ya kukamata madereva pikipiki wanaokiuka sheria hiyo inaendelea katika vituo vyote vya polisi nchini.

"Tumeliona tatizo hilo na tunaendelea kulidhibiti, wito wangu kwa wazazi na walezi waache tabia ya kuruhusu watoto wao kubebwa katika pikipiki chini ya miaka tisa.

"Watoto kama ni wakubwa, abebwe mmoja. Tutawakamata wote wanaobeba abiria zaidi ya mmoja, kwani huo ni ukiukwaji wa sheria, hatutowafumbia macho, kila mara tunatoa elimu kuhusu suala hiya," alisema Ng'anzi.

Kuhusu sheria dhidi ya wazazi wanaoruhusu watoto wadogo kubebwa katika pikipiki na wakati mwingine zaidi ya mmoja, Ng'anzi anafafanua kwamba, sheria iliyoko haimuweki hatiani mzazi.

Anasema kutokana na changamoto hiyo, wanatazama namna ya kuweka kanuni zitakazombana na mzazi moja kwa moja ili kuleta fundisho kwa wengine.

Hata hivyo, Ng'azi anasema kwa kuwa sheria inamzungumzia mwenye pikipiki, wataendelea kushughulika nao kwa sababu wanajua kanuni za uendeshaji barabarani na wanazikiuka kwa kujua.

**Imeandaliwa na Vitus Audax (MWANZA), Neema Emmanuel (MWANZA), Shaban Njia(KAHAMA), Elizabeth Seleman (SENGEREMA)**

*Kwa maoni: +255 677 020 701*
*Email: customerrelations @ guardian.co.tz*



Waziri wa Mifugo na Uvuvi na Mbunge wa Mkuranga, Abdallah Ulega (mwenye kipaza sauti), akizungumza na wananchi waliojitokeza kupata huduma ya matibabu ya macho bure, iliyoandaliwa na taasisi ya Bilal Mission kwa kushirikiana na kampuni ya Yas, jimboni, jana. **PICHA: FAUSTINE FELICIANE**

# Majaliwa asisitiza miiko, maadili kwa wahandisi

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, awataka wahandisi wote kuzingatia miiko na maadili ya taaluma hiyo ikiwamo kutekeleza miradi ya ujenzi kwa ubora unaoendana na thamani ya fedha halisi iliyotolewa.

Majaliwa aliyasema hayo juzi kwenye Kongamano la Kimataifa la 14 la Taasisi ya Wahandisi Tanzania (IET) katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha (AICC), jijini Arusha.

"Sote tunatambua kwamba wako wachache katika taaluma yenu ya uhandisi ambao wanaichafua kwa kufanya matendo ambayo ni kinyume cha taaluma lakini pia ni kinyume cha maadili. Matendo hayo ni pamoja na rushwa, ubadhilifu, na ukosefu wa weledi. Hii si tu kwamba inachafua taaluma ya uhandisi, bali pia inaharibu taswira ya nchi," alisema.

Majaliwa pia aliiagiza Bodi ya Usajili wa Wahandisi (ERB) Kusimamia maadili ya kihandisi na kampuni za kihandisi kwa mujibu wa sheria ili kulinda hadhi ya uhandisi nchini.

Waziri Mkuu alitoa rai pia kwa Taasisi ya Wahandisi Tanzania (IET) kuendelea kushirikiana na vyombo mbalimbali kuwabaini wanaokiuka maadili na sheria na kuchukua hatua stahiki kwa kuwa taaluma ya uhandisi ni muhimu na inapaswa kutunza na kulinda heshima yake. Katika hatua nyingine, Majaliwa alizielekeza mamlaka za serikali za mita na usalama barabarani kuhakikisha kuwa vizuizi na vituo vya ukaguzi vinazingatia usalama wa watumiaji na tahadhari zote za kiusalama.

"Wahandisi na wataalamu wetu mna wajibu wa kuendelea kubuni na kupendekeza mifumo bora ya alama za barabarani, usimamizi wa miundombinu ya barabarana uwekaji wa vituo vya ukaguzi ili kupunguza ajali na madhara yake," alisema.

Naye Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa, alisema serikali imeendelea kufanya maboresho ya kanuni ili kusaidia wakandarasi na wahandisi wazawa kushiriki katika ujenzi wa miradi mbalimbali inayotekelezwa na serikali nchini.

"Kwa sasa thamani ya miradi ambayo haizidi Sh. bilioni 50 inakwenda kwa wazawa na hili kwa kiasi kikubwa imeleta mabadiliko makubwa kwenye sekta ya ujenzi. Pia tumelegeza masharti ya TANROADS (Wakala wa Baranara Tanzania) kwenye ununuzi ili kanuni hii iendane na masharti rafiki pamoja na kuimarisha Kitengo cha usimamizi wa miradi cha TECU kilichoko TANROADS ambapo wameendelea kusimamia miradi kwa viwango na ubora badala ya kutegemea utegemezi wa kampuni za nje," alisema.

Rais wa Taasisi ya Wahandisi Tanzania (IET), Mhandisi Dk. Gemma Modu, alipongeza serikali kwa juhudi za kuongeza ushiriki wa wazawa katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo ambayo kwa kiasi kikubwa inafungua fursa kwa wahandisi wazawa na mafundi wote nchini.

"Kutokana na kasi ya utekelezaji wa miradi mbalimbali, tutaendelea kushirikiana na serikali na tunaahidi kuendeleza na kukuza kiwango cha ujuzi na kusisitiza uzalendo na uadilifu katika utekelezaji wa miradi," alisema.

# Halmashauri zaagizwa kuhamasisha wananchi kutumia miradi kwa tija

**Na James Mwanamyoto,**
SUMBAWANGA

Naibu Waziri, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) anayeshughulikia afya, Dk. Festo Dugange, amezitaka halmashauri zenye miradi yenye kujiendesha kama masoko na stendi kuwahamasisha wananchi kuitumia ili iwe na tija na manufaa kwa jamii na taifa.

Dk. Dugange ametoa maelekezo hayo mjini hapa kwenye ukumbi wa Nazareti, wakati wa hafla ya utiaji saini mkataba wa ujenzi wa soko kuu la mazao ya nafaka ambalo litajengwa eneo la Kanondo kupitia fedha za mradi wa TACTIC.

Alisema wakulima wengi wamekuwa wakipata changamoto ya kutunza mazao katika maeneo ambayo yanaharibika, hivyo ujenzi wa soko hilo na masoko mengine kupitia mradi wa TACTIC umekuja wakati mwafaka.

"Soko hili likikamilika muwe na mpango wa kuwahamasisha na kuwaelimisha wananchi na wakulima ili kulitumia kufanya biashara na kujipatia faida itakayowawezesha kujijenga kiuchumi na kuchangia pato la taifa," alisisitiza.

Dk. Dugange ametaka wakurugenzi wa halmashauri wanaotekeleza miradi ya TACTIC, kuhakikisha mikataba ya utekelezaji inatiwa saini kwa wakati na kusimamia kikamilifu utekelezaji wake.

Alisema Rais Samia Suluhu Hassan ametoa kipaumbele kwa makandarasi wazawa kupatiwa miradi ya TACTIC, hivyo makandarasi hao wanapaswa kutekeleza miradi hiyo kwa ufanisi na uzalendo ikiwa ni sehemu ya kuunga mkono uamuzi wa Rais kuwapatia miradi.

Jumla ya Sh. bilioni 7.4 zitatumika katika ujenzi wa soko kuu la mazao ya nafaka ambalo litajengwa eneo la Kanondo, Manispaa ya Sumbawanga, kwa mujibu wa mkataba uliotiwa saini na linatarajiwa kukamilika Desemba, mwakani.

# Othman: Wanawake mhimili kupigania mageuzi ya kisiasa






**Na Romana Mallya**

MWENYEKITI wa Taifa wa Chama cha ACT Wazalendo, Othman Masoud Othman, amesema wanawake ndio mhimili muhimu katika kupigania mageuzi ya kisiasa na kiuchumi Zanzibar kwa vile wao ndio waathirika wakubwa katika masuala ya kupigania demokrasia nchini.

Othman ambaye pia ni Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar aliyasema hayo Gombani, Chake Chake, kisiwani Pemba wakati akizungumza katika ufunguzi rasmi wa Kongamano la Wanawake wa chama hicho wa mikoa minne ya chama kisiwani Pemba.

Alisema hatua hiyo inatokana na ukweli kwamba, mbali na madhara yanayowakumba wanawake katika harakati za maisha na kisiasa, changamoto nyingi za kiuchumi na kisiasa zinazotokea, wao ndio watu wa mwanzo kupambana nazo, hivyo ni wajibu wao kushirikiana katika kupambania mageuzi kwa maendeleo endelevu kwa wao na taifa kwa jumla.

Aliwataka wanawake hao kutimiza wajibu wao wa kuongoza katika harakati za chama hicho za kupigania kuleta mageuzi, ili kuwapata viongozi bora wenye maono na kuwajibika ipasavyo kwa wananchi na taifa liweze kupiga hatua kimaendeleo.

Othman alisema Zanzibar ni nchi iliyojaaliwa kuwa na rasilimali nyingi zinazoweza kusaidia kuondosha umasikini na jambo muhimu ambalo pia, mataifa kadhaa yamefanikiwa ni kuwapo uongozi bora wenye maono makubwa katika kuzitumia vyema rasilimali zake zilizoko kwa maendeleo ya taifa.

Kwa mujibu wa Othman, dhamira ya chama hicho sio kutafuta vyeo au maendeleo ya chama chao, bali ni kuleta mabadiliko ya kiuchumi na kimaendeleo kwa maslahi ya nchi.

Aliwataka wanawake hao kutochoka na kuhakikisha wanafuatilia vitambulisho vya Mzanzibari kwa mamlaka husika, kwani ndio silaha itakayosaidia kuleta mabadiliko ya kidemokrsia wanayoyataka ndani ya Zanzibar.

Mwenyekiti wa Ngome ya Wanawake ACT Wazalendo, Janeth Rithe, alisema wanawake wanapaswa kuendelea kujituma na kuhamasisha wengine wote na kuutumia wingi wa idadi yao katika kufanikisha kupambania mageuzi yanayohitajika nchini, ili taifa liweze kupata maendeleo ya kweli.

Aliwataka wanawake wa chama hicho kujitahidi kuchukua hatua stahiki katika kuimarisha umoja na uwajibikaji ili kuleta matokeo chanya ya harakati zao za kisiasa.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# *Suala la wasichana kuwa juu kuliko wavulana lisichukuliwe kwa wepesi*

**VUGUVUGU** la mageuzi na harakati za usawa wa kijinsia zimekuwa zikiendelea duniani kote na matokeo makubwa yameonekana huku wanawake wakionekana kuwa katika nafasi za juu za uongozi kwenye serikali, taasisi za serikali na mashirika ya taasisi binafsi.

Hatua hizo za kuwawezesha wanawake kwenye nafasi za uongozi na vyombo vya uamuzi zilianza katika muktadha wa usawa wa kijinsia baada ya kundi hilo kusetwa kwa karne nyingi. Jambo la kwanza, wanawake walikuwa hawahesabiwi wakati wa sense za enzi hizo na hata katika baadhi ya mataifa walikuwa hawaruhusiwi kupiga kura. Hali hiyo ilisababisha mwanamke aonekane kiumbe dhaifu na msaidizi tu wa mwanamume.

Lakini kuanzia mwishoni mwa miaka ya 1940 ndipo lilipotolewa azimio la kimataifa la haki za binadamu ambalo lilisisitiza usawa baina ya wanaume na wanawake. Baada ya hapo wanawake walianza kufikiriwa na kuruhusiwa kushika nafasi za uongozi kwenye serikali na taasisi za kitaifa na kimataifa. Mpango huo ulishika kasi zaidi na hatimaye Mkutano wa Beijing wa mwaka 1995 ulikoleza moto na kuhimiza kuwe na usawa wa kijinsia unaozingatia nafasi sawa katika uongozi kwa maana ya asilimia 50 kwa 50.

Mpango huo ulianza kutekelezwa kwenye mataifa mbalimbali, Tanzania ikiwamo, kwa wanawake kupewa nafasi za juu katika vyombo vya uamuzi. Tangu wakati huo, imeshuhudiwa wanawake wakipewa nafasi kubwa zikiwamo za urais na umakamu wa rais. Katika harakati hizo, hivi sasa Tanzania inaongozwa na Rais mwanamke, Samia Suluhu Hassan ambaye kabla ya hapo alikuwa Makamu wa Rais.

Licha ya nafasi ya Rais, kuna nafasi nyingi ambazo zinashikwa na wanawake katika mihimili ya Bunge na Mahakama. Hivi sasa Bunge linaongozwa na mwanamke ambaye ni Dk. Tulia Ackson akiwa mwanamke wa pili baada ya Anne Makinda. Wawili hao kabla ya kushika nyadhifa hizo, waliwahi kuwa manaibu spika.

Pia katika mahakama idadi ya wanawake imeendelea kuongezeka hali inayoonesha kuwa usawa wa kijinsia unazingatiwa. Pamoja na kuwapo kwa idadi kubwa ya wanawake katika uongozi, pia wengi wao wameonekana kufanya vizuri hata kuwashinda baadhi ya wanaume. Jambo kubwa ambalo pia linasisitizwa kuhakikisha wanawake wanafanya vizuri ni katika elimu ambako watoto wa kike wamekuwa wakipewa nafasi kubwa pamoja na ufadhili katika masomo mbalimbali hususani ya sayansi. Huku nako wameonekana kufanya vizuri na katika matokeo ya mitihani ya sekondari hadi elimu ya juu, wasichana wameanza kuwashinda wavulana.

Suala hilo limeibua mjadala hadi Spika Mstaafu Makinda, kutaka utafiti ufanyike ili kujua sababu za watoto wengi wa kiume kuachwa nyuma kitaaluma na wenzao wa kike.

Makinda ambaye pia ni Mkuu wa Chuo Kikuu cha Kairuki, alitoa hoja hiyo juzi wakati wa Kongamano la Sita Kitaaluma lililoandaliwa na chuo hicho, kujadili namna sekta ya afya inavyoweza kufanya mabadiliko kwa huduma hizo kutolewa kidijitali. Aliweka bayana kwamba siku za karibuni watoto wa kike wameonekana kuongoza kitaaluma na kuwaacha mbali wenzao wa kiume jambo ambalo alisema jamii haipaswi kulifumbia macho na kuliona kama la kawaida.

Kutokana na kuwapo kwa hali hiyo, alisisitiza kufanyika kwa utafiti ili kupata sababu maridhawa na kuhimiza kwamba hali hiyo isiwe ya kuifurahia kwa sababu kuna mambo yanayoweza kujitokeza na kuleta athari kubwa kwa jamii kwa miaka ijayo.

Wazo lililotolewa na Makinda ni la muhimu kwa sababu tangu kuumbwa kwa misingi ya dunia, mwanamume amepewa majukumu makubwa kuanzia ngazi ya familia hadi taifa lakini matokeo yake hivi sasa kuna mabadiliko makubwa. Ni ukweli usiopingika kwamba hata baadhi ya majukumu ya wanaume ndani ya familia yameshikwa na wanawake.

Kama alivyosema Makinda, jamii isilichukulie kwa mtazamo mwepesi suala hilo kwa sababu athari zake mbele ya safari ni kubwa. Ni heri kukinga kuliko kuponya.


Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com







## Muungwana Lazima Nilonge

# Wanaokwepa bei elekezi ya mbolea wabanwe

Na Sabato Kasika

**KILIMO** huwa kinatajwa kuwa ndicho uti wa mgongo wa taifa, ingawa ni cha kutumia jembe la mkono, huku asilimia kubwa ya Watanzania wakijishughulisha na kilimo maeneo ya vijijini.

Wakati kilimo chenyewe kikiwa bado ni cha kusuasua, kimeingiwa na hujuma ambazo kama hazidhibitiwi haraka, wakulima wataendelea kuumia, kwa kutumia nguvu na kujikuta wasipate mazao ya kutosha.

Serikali imejitahidi kusaidia wakulima kuzalisha kwa ufanisi kwa kuipa jukumu Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) jukumu la kutoa bei elekezi kwa wafanyabiashara wa mbolea.

TFRA inafanya kazi hiyo ikitegemea kuwa wafanyabiashara watatimiza jukumu hilo kikamilifu kama inavyotakiwa, lakini baadhi yao wanatuhumiwa kukwepa bei elekezi.

Kitendo hicho cha kukwepa bei elekezi ni sawa na kuwaumiza wakulima ambao kimsingi maisha yao yanategemea kilimo, lakini mazao yanayotokana na kilimo hicho wanayotumia wakazi wa mijini.

Maeneo mbalimbali ya nchi, kumekuwa na malalamiko kutoka kwa wakulima kuhusu bei kwamba wanabambikiwa bei kubwa isiyoendana na ile iliyoelekezwa na serikali ambayo hawawezi kuimudu.

Wafanyabiashara wenye mchezo wangedhibitiwa ili wasiendelee kuumiza wakulima, kwani kuendelea kwao kunaumiza nchi nzima wakiwamo wale ambao si wakulima lakini wanategemea kununua mazao.

Serikali imebeba dhamana ya ruzuku ya mbolea ya wakulima lakini wanajitokeza wajanja wachache na kuhujumu dhamana hiyo ya kusaidia wakulima ili wazalishe mazao mengi shambani.

Kama ambavyo serikali iliweza kuwadhibiti wafanyabiashara waliokuwa wakiuzia wakulima mbolea feki, ifanye hata kwa hao wanaowapandishia wakulima bei kwa lengo la kujinufaisha.

Nakumbuka miaka ya nyuma kulikuwa na malalamiko kutoka kwa wakulima kuwa wanauziwa mbolea feki kama saruji, majivu na vitu yakiwa yamechanganywa na mbolea kidogo.

Matokeo yake ikawa inaharibu mazao, sasa wamekuja na mtindo mwingine wa kuacha bei elekezi na kuweka wanayojua wenyewe.

Yote hayo ni kutaka kujipatia fedha nyingi kwa mbinu ovu.

Ikumbukwe serikali inasema mipango na mikakati yake ni kutaka ifikapo mwaka 2030, sekta ya kilimo iwe imesonga mbele kwa asilimia 30, ikilinganishwa na ya sasa ambayo ni asilimia 3.6.

Baadhi ya mambo ambayo Rais Samia Suluhu Hassan anayaainisha na yanayotazamwa kama nguzo katika kuchochea ukuaji huo, ni pamoja na mageuzi yanayoendelea kufanywa ndani ya sekta ya kilimo kama vile uanzishwaji mpango wa vijana kujikita kwenye kilimo na ongezeko la kiwango cha bajeti katika sekta hiyo.

Kwa mujibu wa Rais, bajeti hiyo ya kilimo kwa mwaka wa fedha 2022- 2023 iliongezeka mara nne ikilinganishwa na ile iliyopita. Ongezeko hilo limeifanya serikali kuwa na uwanja wa kuanza kutoa ruzuku ya mbolea kwa wakulima.

Wakati serikali ikitoa ruzuku ya mbolea kwa wakulima, ni vyema mbinu zote za wanaokwepa bei elekezi zidhibitiwe na ikiwezekana wanyimwe vibali vya kusambaza mbolea hiyo kwa wakulima.

Lakini pia wale ambao huwa wanatuhumiwa kuvusha mbolea na kwenda kuiuza katika nchi za jirani, nao wafuatiliwe, kunaswa na wadhibitiwe ili wasiendelee kuumiza wakulima.

Kwa miaka mingi sekta ya kilimo imekuwa ikijikongoja, kutokana uwekezaji mdogo, lakini safari hii wakulima wamepata matumaini mapya kutokana na jitihada zilizofanywa na serikali.

Jitihada za serikali zisivurugwe na wafanyabiashara wachache wenye nia mbaya ya kutaka utajiri wa haraka bila kujali madhara yatokanayo na mchezo wao huo ambao ni hatari kwa kilimo.

Hivyo, wanaokwepa bei elekezi ya mbolea waendelee kubanwa hadi waachane na mchezo wao, au wale wanaobainika kujihusisha na hujuma hiyo wanyang'anywe leseni.

**MAKALA**

**FIKRA MBADALA**

# Viongozi zingatieni kitu kinachoitwa kibali



Pascal Mayalla

HABARI zenu Watanzania wenzangu na wazalendo kwa nchi yetu. Leo nimeona vyema niendeshe somo la kitu kinachoitwa "Kibali".

Katika somo hilo, jambo la kwanza tujifunze nini maana ya kibali. Pamoja na kujua maana ya neno hilo, pia tutaona kibali kina kazi gani, kibali kina sifa gani na mtu akikitumia vyema atapata matokeo gani na pia mtu asipokitumia vyema nini kitamtokea.

Mambo mengine ya kujifunza ni je, kibali kinatolewa kwa nani?Anayepewa kibali anajua kuwa ana kibali? Na utamjuaje mtu mwenye kibali?

Kwanza kabisa, kibali ni ruhusa ya kufanya jambo fulani ambalo ili ulifanye ni lazima uruhusiwe na mamlaka husika. Kibali kikuu cha kwanza kwa binadamu baada ya kuumbwa ni uhai kibali cha kuishi na cha kuumba binadamu wengine.

Baada ya hapo ni kibali cha kufanya kila kinachofanyika. Kibali kwa mwanamke kuwa mama na mwanamume kuwa baba ni kupevuka na kibali cha kujenga familia ni kuoa. Kibali cha kujenga nyumba ni kumiliki ardhi kufanya biashara ni kuwa na leseni kusafiri nje ni kuwa na pasipoti na kuingia nchi fulani ni kuwa na visa. Hivyo ni baadhi ya vibali lakini viko vya aina nyingi.

Kibali ninachokizungumza kwenye uga huu ni cha uongozi na utumishi wa watu, hivyo nawazungumzia viongozi. Kuwa na kibali ni cha kutimiza lile jukumu la kibali ulichopewa. Kama ilivyooneshwa katika maana ya kibali, kuna aina tofauti ambavyo vinaruhusu kufanya mambo tofauti tofauti. Ukipewa kibali cha ndoa huna budi kutimiza majukumu ya ndoa na ukipewa kibali cha kufanya biashara unafanya biashara kwa mujibu wa leseni yako.

Kwa maana hiyo, hata kibali cha uongozi wa nchi kiongozi anatakiwa kutawala kwa mujibu wa kibali alichopewa. Japo kibali cha kutawala nchi kimetolewa kwa mujibu wa katiba kwa kiongozi kuchaguliwa kwa kupigiwa kura, anayeshinda anakuwa amepata kibali kutoka kwa YEYE (Mungu) na anapaswa si tu kufuata katiba bali pia kutimiza madhumuni ya YEYE aliyempa kibali hicho. Pia anatakiwa kutambua amepewa kibali cha nini, ili afanye nini na kibali chake ni cha muda gani.

Sifa za Kibali

Kibali kina sifa kuu tano ambazo ni kwamba kinatolewa na Mungu, kina kazi mahsusi, kina muda maalum, kikitumika ipasavyo aliyepewa kibali anafanikiwa na mwisho, kisipotumika kwa madhumuni yaliyokusudiwa kinafutwa.

Musa, kwa mfano, kibali chake kilikuwa kuwakomboa tu wana wa Israel kutoka utumwani Misri. Alipokamilisha kazi ya kuwaondoa na kuwasafirisha kwenda nchi ya ahadi, kibali chake kikakamilika. Musa hakuingia nchi ya ahadi, alitwaliwa, na kibali cha kuwaingiza nchi ya ahadi, kikatolewa kwa mtu mwingine.

Kwa vile kibali ni cha kazi maalum kwa mtu maalum, kwa muda maalum, ukiwa na kibali, usipokitumia kikamilifu, kibali hicho kinafutwa na usipokamilisha kazi ya kibali chako katika muda uliopangwa, kibali hicho kinakwisha muda wake.

Kibali kinatolewa na nani

Vibali vinatolewa na mamlaka husika kutegemeana na aina ya kibali chenyewe na cha aina gani. Kama nilivyosema awali, kuna vibali vya aina mbili, vya shughuli za kidunia, vinavyotolewa na mamlaka za kidunia, na vibali vya mambo makuu, vinatolewa na mamlaka kuu ambayo ni Mungu. Mtu unakuwa umepata kibali machoni mwake. Vibali vya YEYE mwenyewe, mtu haombi, anazaliwa nacho au unapewa na YEYE mwenyewe kwa madhumuni mahususi.

Mfano, urais wa nchi hupatikana kwa kuomba kuteuliwa. Waombaji wanakuwa wengi lakini anayepata ni mmoja. Huyo mmoja anayefanikiwa kupata, anakuwa ndiye mwenye kibali kutoka kwa YEYE. Mungu anakuwa na madhumuni fulani kwa nini amempa kibali huyo aliyempa.

Kati ya wagombea wote wanaogombea, mwenye kibali ndiye hushinda. Kwa vile kibali kinatolewa na Mungu mwenyewe, kinatolewa kwa yule Mungu aliyemchagua.

Mara nyingi kwenye familia zetu, kwa mfano, baba ndiye huhesabika ni kichwa cha familia. Tangu Mungu alipomwumba Adam, alimpa kibali cha kutawala viumbe vyote vya dunia hii. Japo baba ndiye anapaswa kuwa kichwa cha familia, kuna familia nyingi, mama ndiye anakuwa amepewa kibali, hivyo ndiye kichwa cha familia.

Familia nyingi pia huwa zinapenda mtoto wa kwanza awe mwanamume ili apewe kibali cha mzaliwa wa kwanza lakini kuna nyingi mzaliwa wa kwanza ni mtoto wa kike, hivyo anapata kibali cha uzaliwa wa kwanza.

Kwa vile kibali kinatolewa na Mungu mwenyewe, si lazima mzaliwa wa kwanza apate kibali. Mungu anaweza kumteua mtoto yeyote na kumpa kibali. Mfano, japo mzaliwa wa kwanza wa Adam ni Kaini, kibali kilitolewa kwa mdogo wake Abeli (Habili), Japo mzaliwa wa kwanza wa Nabii Ibrahim ni Ismail, aliyepewa kibali ni mzaliwa wa pili Isaka. Na kwa Isaka, japo mzaliwa wa kwanza alikuwa Essau, aliyepata kibali ni Yakobo. Yakobo yeye alipata watoto 12, mtoto mwenye kibali alikuwa Yusufu, mzaliwa wa 11. Na Daudi katika familia ya Yese ndiye alipewa kibali.

Kwa hiyo, kibali kinaweza kutolewa kwa yeyote, anayeamua nani apewe kibali ni YEYE. Hata kwenye imani zetu za kiasili, watoto wanakuwa na vipawa mbalimbali na anayechaguliwa kurithi mikoba, anaweza kuwa mtoto wa mwisho. Hicho ndicho kibali.

Tukutane wiki ijayo kwa mwendelezo wa somo hili.

**Wasalaam,**
**Paskali**
**0784270403**

**KONA YA AFYA**

# Maswali yanayoulizwa zaidi kuhusu shinikizo la damu



Na Dk. Mabula Budodi

SHINIKIZO la damu ni moja ya magonjwa yasiyo ya kuambukiza ambayo yanaisumbua jamii kwa kiasi kikubwa kwa sasa. Kutokana na kutamalaki kwa ugonjwa huo, kumekuwa na maswali kadhaa yanayoulizwa na watu. Maswali hayo ni;-

Mosi, Mambo gani yanayosababisha kupata shinikizo la damu? Sababu halisi haijulikani lakini mambo kadhaa huweza kuchangia. Mambo hayo ni vinasaba vya mwili, yaani kurithi shinikizo la damu kutoka kwa wazazi kama wana tatizo hilo; kutokufanya mazoezi; unene uliopitiliza; kuvuta sigara; kunywa pombe; kula chakula chenye chumvi nyingi; umri mkubwa; msongo wa mawazo wa muda mrefu; na magonjwa mengine pia kama tatizo la figo, sukari na hata vichochezi mwili yaani homoni.

Pili, dalili gani huashiria kuwa na shinikizo la damu? Shinikizo la damu (presha) huitwa muuaji wa kimya kimya kwa sababu halina dalili za moja kwa moja zinazoweza kuashiria kwamba sasa umeshapata tatizo hilo.

Mara nyingi mtu mwenye shinikizo la damu huwa hajisikii vizuri ndiyo maana ni muhimu kupima presha kama una viashiria vya kupata tatizo hilo.

Baadhi ya dalili zinaweza kuwa kichwa kuuma sana, kifua kuuma, kupoteza uwezo wa kuona, yaani uoni hafifu, kushindwa kupumua na kutapika. Lakini si siku zote na kwa wakati wote dalili hizi hutokea.

Tatu, nawezaje kugundua kama nina shinikizo la damu? Jibu ni kwamba shinikizo la damu huweza kugunduliwa kwa kupima presha mara kwa mara kwa wataalamu wa afya angalau mara mbili kwa saa tofauti tofauti au kupima mara kadhaa ndani ya majuma machache.

Nne, je, presha ya kawaida ni ipi? Katika Jarida la Umoja wa Mataifa (UN) kuhusu kuzuia, kutambua na kutibu, suala la shinikizo la damu limegawanywa katika makundi kadhaa. Kundi la kwanza ni presha ya kawaida ambayo presha ya juu ya kipimo cha presha ni 120 na ya chini ya kipimo kuwa 80. Kundi la pili, presha iliyopanda, yaani presha ya juu, kuwa 120 hadi 129 na presha ya chini kuwa chini ya 80.

Hatua ya kwanza ya shinikizo la damu, presha ya juu kuanzia 130-139 na presha ya chini kuwa 80-89. Hatua ya pili ya shinikizo la damu, presha ya juu huwa 140 au zaidi na presha ya chini kuwa 90 au zaidi.

Tano, vyakula gani napaswa kutumia katika shinikizo la damu? Mfumo wa ulaji wa chakula husaidia kupunguza hata kuzuia tatizo la shinikizo la damu kama hujapata. Kula matunda zaidi, mboga na vyakula vyenye mafuta kidogo kama maziwa, mayai na karanga.

Pia kupunguza au kuacha kutumia mafuta yanoweza kuganda katika joto la chumba yaani mafuta ya wanyama na lehemu vinavyopatikana kwenye vyakula vya kukaangiza zaidi.

Punguza nyama nyekundu na vitu vitamu, kula chakula kilicho na viwango vingu vya maginiziamu, potasiumu na kalisiumu. Pia Punguza ulaji wa chumvi kwenye chakula.

Sita, je, naweza kupunguza presha bila kutumia dawa? Ni kweli. Unaweza kupunguza tatizo la kupaunda kwa presha kwa kubadili mfumo wa maisha kama kuacha kunywa pombe, uvutaji wa sigara, kufanya mazoezi, kupunguza ulaji chumvi na pia kupunguza msongo wa mawazo. Hii hutumika pekee pekee kwa watu ambao hawana kiwango kikubwa cha presha na kwenye hatua za awali za shinikizo la damu.

Kwa wale wenye presha kubwa huhitajika kutumia vyote kwa pamoja, yaani kubadili mfumo wa maisha na matumizi ya dawa ili kuzuia madhara yanayoweza kusababishwa na tatizo hilo. Saba, je, naweza kupona shinikizo la damu kama nikitumia dawa? Shinikizo la damu(presha) huweza kudhibitiwa na kumudiwa na madadiliko wa mfumo wa maisha unaoendana na shinikizo la damu pamoja na matumizi ya dawa.

Hata hivyo, hakuna tiba inayoweza kuponya kabisa shinikizo la damu. Inakupasa kutumia dawa vizuri na kufata kufanya kama ulivyoelekezwa na mtaalamu wa afya.

Nane, ni salama kumeza dawa za presha na hakuna madahara yanayosababishwa na dawa hizo>? Ndiyo. dawa ulizopewa na dakitari kwa ajili ya kudhibiti shinikizo la damu ni salama na njia sahihi ya kuimudu presha yako kwa punguza uwezokano wa kupata madhara yanayosababishwa na shinikizo la damu.

Tisa, , nifanyeje kama presha yangu iko juu au imepanda?

Kama presha yako iko juu au imepanda sana, ni vyema umwone mtaalamu wa afya akushauri na kutoa uamuzi sahihi kuhusu matibabu. Hii inaweza kuhusiha kubadili dawa, kuongeza dozi kwa pale inapotakiwa ili kuzuia madhara kama kiharusi, matatizo ya moyo na kushindwa kuona.

Kumi, je, naweza kuishi maisha ya kawaida nikiwa na shinikizo la damu?

Ndiyo, kwa kufuata mfumo wa maisha unaotakiwa na matibabu sahihi unaweza kuishi maisha ya kawaida. Muhimu ni kufuatilia presha yako kwa kupima mara kwa mara, kutumia dawa na kubadili mfumo wa maisha.

Pia jaribu kuwa karibu na mtaalamu wako wa afya, yaani dakitari kwa ajili ya kupata ushauri sahihi wa tatizo lako la shinikizo la damu. Kubwa Zaidi, fuata ushauri wa dakitari na matumizi mazuri ya dawa pamoja na kufanya mazoezi ya mara kwa mara.

**• Dk. Budodi ni daktari jijini Dar es Salaam. Anapatikana kwa namba ya simu 0710980096 na baruapepe: " mabilabudodi@gmail.com**

# ACT - Wazalendo yataka wanachama wake waachiwe huru

**Na Restuta James**

WAKATI Chama cha ACT-Wazalendo, kikitaka viongozi na wanachama wake zaidi ya 38 waliokamatwa katika Uchaguzi Serikali za Mitaa kuachiwa bila masharti, Jeshi la Polisi limejibu kwamba, watu hao wanashikiliwa kwa kutenda uhalifu wa kijinai.

Jana, Naibu Katibu wa Haki za Binadamu na Vyombo vya Uwakilishi wa Wananchi wa chama hicho, Mbarala Maharagande, alisema wanachama wake wananyanyaswa kisiasa, kwa kunyimwa uhuru wa maoni.

Alimwomba Rais Samia Suluhu Hassan kulielekeza Jeshi la Polisi kuwaachia viongozi na wanachama wanaoshikiliwa, bila masharti ya kutakiwa kuripoti vituoni mara kwa mara.

Kadhalika chama hicho kikitaka Jeshi la Polisi liwakamate makada wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), waliohusika kuwapiga baadhi ya wafuasi wa ACT-Wazalendo.

Maharagande alisema kumekuwa na matukio ya ukiukwaji na uvunjifu wa haki za binadamu nchini kabla na baada ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Vijiji na Vitongoji uliofanyika mwishoni mwa mwezi uliopita, ikiwamo makada wake kukamatwa, kupigwa, kuteswa na kuumizwa.

Alidai Jumanne wiki hii, watu wasiojulikana, walibandika barua za vitisho katika maeneo mbalimbali ya Kata ya Ruhuhu, wilayani Ludewa, Mkoa wa Njombe, lakini katika hali ya kushangaza, viongozi saba wa ACT-Wazalendo, walikamatwa kwa kuhusishwa na vitisho hivyo. "Askari walivamia Kata ya Ruhuhu na kukamata watu kwa kuvunja milango ya nyumba za wananchi na zaidi kuwalenga wafuasi wetu na kuwalazimisha kuvaa sare za chama kabla ya kuwapeleka kituoni," alidai Maharagande.

Alisema katika tukio lingine, wanachama wake 10 kutoka Kata ya Kagunda, jimbo la Kigoma Kaskazini na 20 kutoka Kata ya Rugongwe, jimbo la Muhambwe, mkoani Kigoma, wanashikiliwa tangu siku ya uchaguzi, Novemba 27, 2024.

Alisema wanachama na viongozi hao wanashikiliwa kwa tuhuma za kuharibu nyaraka za Mtendaji wa Kijiji cha Kaguna.

"Aidha, zaidi ya wanachama na viongozi wetu 200 wamekimbia makazi yao katika Kata za Pamila, Matendo, Nkungwe, Mgaraganza na Kigoma Mjini kutokana na kuogopa vitisho, kupigwa na kukamatwa na askari wa Jeshi la Polisi," alifafanua. Alisema matukio mengine ni kukamatwa na kupigwa kwa viongozi wa chama hicho ngazi mbalimbali, akiwamo Mwenyekiti wa chama hicho, Mkoa wa Songwe, Ezekia Zambi, Makatibu wa majimbo ya Igunga, Elick Yugalila, na Ulyankulu, Zakaria Lugembe, pamoja na uharibifu wa mali za wanachama katika maeneo mbalimbali.

**MAJIBU YA POLISI**

Akizungumza jana na mwandishi wa Habari hii, Msemaji wa Jeshi la Polisi, Naibu Kamishna (DCP) David Misime, alisema polisi hawamkamati mtu kwa sababu za rangi, dini wala ufuasi wa chama cha siasa.

"Mtu hukamatwa kwa sababu ya tuhuma za jinai zilizowasilishwa kituoni dhidi yake au kama atakuwa anatenda uhalifu akakamatwa eneo la tukio. "Waliokamatwa kutoka katika wilaya zilizotajwa kulikuwa na malalamiko dhidi yao ya kutuhumiwa kutenda uhalifu wa kijinai," alisema DCP Misime.

"Baadhi walishafikishwa mahakamani na wengine wapo nje kwa dhamana wakisubiri taratibu za kukamilisha upelelezi zikamilike ili hatua zingine za kisheria zifuate.

"Tunatoa wito kwa baadhi ya viongozi wa kisiasa wanapotoa taarifa zao watoe ufafanuzi wa kueleweka na wa ukweli," alisisitiza DCP Misime



Sehemu ya vijana wa Tanzania walioshiriki kambi ya utafiti, Shenzhen, China. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Wanafunzi Tanzania washiriki kambi ya utafiti China

**Na Mwandishi Wetu**

WANAFUNZI wa Tanzania wameshiriki kambi ya utafiti wa vipaji vya kidijitali ya Huawei Kusini mwa Jangwa la Sahara nchini China.

Shenzhen, China Huawei kwa mara nyingine imedhihirisha dhamira yake ya kuwawezesha vijana wenye vipaji katika nyanja za Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati (STEM) kwa kuandaa Kambi ya Utafiti wa Vipaji vya Kidijitali ya Huawei kutoka nchi za Afrika.

Nchi hizo ni zile zilizoko Kusini mwa Jangwa la Sahara (LEAP) lililofanyika kuanzia Novemba 18 hadi 22, 2024 nchini China .

Mpango huo wa kidijiti umedhamiria kutoa maarifa ya uongozi na kutoa uwezekano wa fursa za kuajiajiri ukilenga zaidi (LEAP) kukuza stadi za juu katika tasnia ya kidijitali na kukuza uvumbuzi miongoni mwa vipaji vya vijana kutoka kanda ya Afrika.

Kambi hiyo iliyofanyika katika makao makuu ya kimataifa ya Huawei huko Shenzhen, ni sehemu ya dhamira pana ya Huawei ya kuendeleza wafanyakazi wenye ujuzi katika anga za kidijitali kote barani Afrika.

Aidha, kambi hiyo ilileta pamoja wanafunzi wenye vipaji vya kipekee kutoka nchi 17 za Afrika zilizopo Kusini mwa Jangwa la Sahara, ikiwa ni pamoja na Tanzania, Nigeria, Afrika Kusini, Mauritius na Kenya.

Kambi hiyo ya utafiti iligusa ajenda muhimu za kidijito ikijumuisha kozi za ICT kuhusuc teknolojia ya kisasa kama vile Akili Mnemba (AI), mawasiliano ya mtandao wa 5G, nguvu za kidijitali, teknolojia za masafa pamoja na kongamano la uongozi.

Tukio hilo la wiki moja lilifikia kilele kwa kuandaliwa shindano la Tech4Good na washiriki kutoka nchi tofauti waliunda timu ili kuja na majawabu kupitia teknolojia yanayojibu changamoto za kijamii.

Tanzania iliwakilishwa na wanafunzi 10 bora kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Dodoma na Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam (DIT). Huawei ilitoa ufadhili kamili kwa safari za ndege za kwenfa na kurudi, malazi, na mafunzo kwa washiriki wote, ili kuhakikisha kwamba umakini wao unabaki kwenye kujifunza

Kambi ya Utafiti wa Vipaji vya Kidijitali ya LEAP, ilizinduliwa na Huawei katika nchi za Afrika zilizoko Kusini mwa Jangwa la Sahara mwaka 2022 ikiwa ni sehemu ya mpango wake mpana wa kukuza wafanyakazi wenye ujuzi katika anga za kidijitali kote barani Afrika.

Huawei inatazamiwa kuinua dhamira yake ya kuendeleza vipaji vya kidijitali katika Afrika nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara kwa kutoa mafunzo kwa vijana 150,000 kupitia mpango wake wa kukuza ujuzi wa kidijitali wa LEAP katika miaka mitatu ijayo.

Mpango huo ni sehemu ya mkakati mpana wa Huawei wa kuwekeza katika rasilimali za kimataifa zinazolenga kukidhi mahitaji mahusus ya vipaji vya

## Wataka utafiti bidhaa mazao uvuvi kuongeza thamani zaidi

**Na Romana Mallya**

SERIKALI imeelekeza Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini kufanya utafiti wa bidhaa za mazao ya uvuvi, hususani kwa Ziwa Victoria ambalo kwa sehemu kubwa linagusa wananchi wengi wa Kanda ya Ziwa, ili kuibua miradi ya kuongeza thamani ya mazao ya uvuvi.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha, Elijah Mwandumbya, aliyasema hayo kwa niaba ya Waziri wizara hiyo, Dk. Mwigulu Nchemba, katika Mahafali ya 38 ya chuo hicho, duru ya pili Kituo cha Mafunzo cha Kanda ya Ziwa, Kisesa, mkoani Mwanza, yanayofanyika kwa mara ya 12 katika Kituo hicho.

Alisema serikali itaendelea kuwajengea uwezo wavuvi na wafugaji wa samaki ili waongeze uzalishaji, kuzalisha ajira, kuimarisha usalama wa chakula, kuongeza kipato cha wavuvi na watu walioko katika mnyororo wa thamani na hivyo kuchangia kwenye Pato la Taifa.

"Eneo linalopewa uzito wa hali ya juu na serikali ni pamoja na elimu biashara, ufugaji wa nyuki, uvuvi, ufugaji wa mifugo, kilimo cha mazao ya nafaka pamoja na uongezaji wa thamani ya bidhaa zikiwamo za uvuvi, kilimo, mifugo pamoja na madini", alisema.

Mwandumbya aliuagiza uongozi chuoni hapo kuangazia sekta ya madini hasa ikizingatiwa kuwa ukuaji wa sekta hiyo umeongezeka na kuajiri vijana wengi.

Alisema kwa mujibu wa Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025, inakadiriwa mchango wa sekta ya madini katika Pato la Taifa, utaongezeka na kufikia asilimia 10 au zaidi kufikia mwaka 2025.

Alisisitiza kuwa madini ni eneo ambalo chuo kinapaswa kuliangalia kwa jicho la aina yake na kushiriki kuchagiza uchumi wa taifa kupitia utafiti endelevu na shirikishi za uongezaji wa thamani ya madini.

Alilipongeza Baraza la Uongozi wa Chuo kwa kuendelea kukisimamia vyema chuo kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa.

Mwandumbya aliwaeleza wahitimu kwamba, ujuzi walioupata watautumia katika kuleta ufumbuzi wa changamoto mbalimbali za maendeleo zinazoikabili jamii.

Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Hozen Mayaya, alisema chuo kimejizatiti katika kuandaa wataalamu wenye weledi wa kutosha katika fani za mipango ya maendeleo, kujenga moyo wa uzalendo na uadilifu kwa wataalamu hao ambazo ni nyenzo za msingi wa maendeleo na ustawi wa nchi.

# MAISHA

DESEMBA 8, 2024

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

Jumapili




Ukurasa 13


**Tamba na Mama Samia**



Ukurasa 15

**MAISHA NI NYUMBA**

Nyumba yako inaonekanaje msimu wa sikukuu?



Ukurasa 12

**SEND OFF**




# Makunyanzi sio tatizo ukifuata njia hizi za asili

Ukurasa 14

# WATOTO

## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA




| | | | |
|---|---|---|---|
| 4 | 3 | 2 | 1 |
| 2 | 1 | 4 | 3 |
| 3 | 4 | 1 | 2 |
| 1 | 2 | 3 | 4 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| T | I | G | E | R | |
| | | O | | | |
| | H | A | W | K | |
| R | A | T | | | H |
| | R | | | | E |
| P | E | G | I | O | N |

## FUMBO TOTO

Hapa umepewa majina ya miji mikuu, jaza katika viboksi vilivyowazi majina ya nchi zake.


LUANDA, MADRID, LOME, BAMAKO, ACCRA, NEW DELHI, KHARTOUM, TUNIS



## TOA TOFAUTI 5



## PAKA RANGI




## AMSHA AKILI

HAYA WADOGO ZANGU, TUENDELEE NA AMSHA AKILI IITWAYO SUDOKU. JAZA NAMBA MOJA MPAKA NNE KWA KILA MSTARI IWE KUTOKA CHINI MPAKA JUU AMA KUSHOTO KWENDA KULIA. HAKIKISHA NAMBA ZINAZOFANANA HAZIGONGANI KATIKA MSTARI MMOJA. KAZI KWAKO!

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | 4 | |
| | | | 2 |
| 2 | 1 | | |
| | 3 | | 1 |

## CHEKA



Alichokifanya daktari

MTOTO John alikuwa na kaweaida ya kwenda mtoni kuoga peke yake. Siku moja akiwa njiani alikutana na bibi mmoja akiwa anaokota kundi kando ya barabara akiwa peke yake.

John alimuhurumia yule bibi na kuanza kumuuliza

**John:** bibi shikamoo

**Bibi:** Marhabaa mjukuu wangu

**John:** Mbona unaokota kuni katika pori hili peke yako, wajukuu zako wako wapi wakusaidie?

**Bibi:** Mjukuu wangu niko hapa porini peke yangu, kama wewe unavyokwenda mtoni ukiwa peke yako

**John:** Ulijuaje bibi kama naenda mtoni kuoga?

**Bibi:** Nimejua kama wewe ulivyojua naokota kuni hapa, lakini sisi wote tunafanya vitendo vya hatari

John alishtka na kuangalia nguo zake alizoweka begani, kisha akakimbia kurudi nyumbani

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Unamwacha mke wa ngekewa, unaoa mke nuksi

***KARIBU tena masomaji wangu Maisha Ndivyo Yalivyo, tuendelee na vimbwanga vya safu hii. Ujumbe katika makala ya leo unajaribu kuonyesha jinsi mtu anavyoweza kuoa au kuolewa na mtu anayerudisha nyuma maendeleo ya familia badala ya kuinyanyua kiuchumi.***

Kwa mfano, yuko jamaa yangu mmoja alikuwa na maendeleo mazuri sana katika shughuli zake za biashara. Mama alikuwa mfanyabiashara za nguo na mume alikuwa mhandisi wa ujenzi. Jamaa huyu alichoamua na mkewe ni kununua viwanja na kujenga nyumba kadhaa za kupangisha.

Alikuwa na mkewe aliyempenda sana. Walibahatika kuzaa watoto watatu. Ni familia iliyoanza maisha katika mazingira magumu ya kuhangaika lakini kutokana na jitihada kubwa za kutafuta, Mungu akawafungulia na kujikuta shughuli zao za biashara zikishamiri.

Kutokana na hatua mbalimbali za mafanikio, wakabuni mradi wa kununua viwanja na kujenga nyumba za kupangisha. Waliweza kujenga nyumba tatu za kupanga na ya nne wakawa wanaishi wenyewe na watoto wao.

Baba huyu mhandisi alipata kazi nyingi za ujenzi, fedha nazo zikakubali. Akaanza kuisahau familia yake na kuanzisha mahusiano holela na wanawake nje ya ndoa. Unajua tena mtu mwenye fedha anavyonaswa na ibilisi ndani ya moyo wake. kila mwanamke apitaye mbele yake anaona ni halali yake kwani anaweza kumnunua kijumla jumla.

Naam. Taratibu baba huyu akaanza vituko, mara anarudi nyumbani mlevi, tena usiku wa manane na wakati mwingine hurejea asubuhi. Ugomvi ndani ya familia hii ulikuwa mkubwa hata kufikishwa kwenye baraza la usuluhishi.

Hata hivyo, kutokana na mke huyu kuathirika kisaikolojia, aliomba kwenye usuluhishi atengane na mumewe na kugawana mali. Suala hili liliamuriwa lifikishwe mahakamani. Huko mahakamani, baada ya ushahidi wa pande zote mbili kutolewa, hatimaye mama alipata talaka yake wakagawana mali.

Mama alipata nyumba moja, nyingine iliamuliwa iwe mali ya watoto. Kuanzia wakati huo, kila mtu akawa na hamsini zake ila malezi ya watoto kila upande ulipewa jukumu lake.

Tokea hapo baba yule inasemekana alianza kubadilisha wanawake kama nguo za kuvaa. Hatimaye alitulia na mmoja. Si unajua tena ule msemo kwamba 'ukichagua sana nazi utaambulia koroma'. Wengine husema, 'adhanie amepata kumbe amepatikana'.

Akaishi na mwanamke yule miaka miwili bila dalili ya kupata mtoto. Tenda za shughuli za ujenzi zikaanza kupungua. Kazi zikitoka akiomba anaenguliwa. Huo ukawa mwanzo wa kuporomoka kiuchumi kwa baba huyu. Akaanza kutumia akiba zake za benki kutanua na mwanamke.

Haukupita muda, wawili hawa wakaanza kugombana kutokana na mahitaji kupungua kwa kasi. Fedha za benki zinatoka tu hakuna zinazoingia ziongezeke. Jamaa akaanza kutafuta mnunuzi wa nyumba mojawapo, akaiuza mil.19/= ghafla akawa tena tajiri.

Hata hivyo, fedha hizi hakuziingiza kwenye mradi wa maendeleo, yeye na mkewe wa pili wakawa wanafanyia matanuzi, nazo zikaisha. Akageukia nyumba anayoishi nayo akaiuza. Akaenda kuomba hifadhi kwa kaka yake mkubwa. Kaka huyu alimhifadhi kwa muda lakini napo akaona ni mzigo kutokana na nduguye kutochangia chochote hata chakula alichokuwa anakula na mkewe.

Kutokana na masimango kuzidi, jamaa inasemekana hivi karibuni na amahemia kwenye chumba ndani ya nyumba ya wageni (gesti). Kama siyo kuchezea shilingi choo ni kitu gani? Mungu anakupa mke au mume mwema lakini wewe unaona kama siyo kitu kwako.

> **"Mama alipata nyumba moja, nyingine iliamuliwa iwe mali ya watoto. Kuanzia wakati huo, kila mtu akawa na hamsini zake ila malezi ya watoto kila upande ulipewa jukumu lake.**

Angalia baba huyu alivyoanza na neema enzi mke wa kwanza. Yule ndiye aliyekuwa mke kwa maisha yake na wala siyo huyu wa pili ambaye baada ya kumuoa hata vile alivyokuwa navyo vikatoweka vyote kwa mfululizo. Unatoa neema na baraka nyumbani unakaribisha nuksi!

Je, baba huyu ataomba msaada kwa nani wakati hata mkewe wa kwanza aliyemfungulia riziki alimdharau? Mkewe mambo yalimyookea tokea alipoachana na mumewe. Yeye ndiye anayetunza watoto kutokana na shughuli zake kushamiri. Hakika jambo usilolijua ni kama usiku wa kiza.

Wachagga wanao msemo kuwa 'Samanya ekesonguo pfo', yaani jambo litakalokutokea mara nyingi huwezi kulijua kabla. Laiti angelijua kuwa mke wa riziki alikuwa ni yule aliyemtaliki, asingechukua uamuzi wa kuoa mwanamke mwingine. Tujifunze kutokana na makosa ya wenzetu. Maisha Ndivyo Yalivyo.

***Je, una maoni, kisa cha kimaisha? Ujumbe mfupi 0715268581. namba hii ipo WhatsApp.***

## WARAKA WA NDANI
Na Godfrey Mushi

# Ukatili huu ni janga jipya nchini

UNAPOZUNGUMZA na mtu yeyote ambaye ameathiriwa na masuala ya ukatili wa kijinsia, tilia mkazo sana lugha yake ya mwili (body language).

Aidha, sikiliza kwa makini zaidi midondoko ya sauti yake au msikilize kwa umakini, huku ukielekeza macho yako kwake muda wote.

Vilevile, uruhusu mwili wako na akili yako, ikupe sura ya upole unapofanya kazi hiyo ya mahojiano na mtu au watu walioathiriwa na ukatili wa kijinsia. Hapo utagundua au kubaini vitu vingi kwa haraka hata kama hawezi kuvisema au kutamka moja kwa moja.

Ndiyo! Kuna utafiti unaonesha kwamba hisia, kupendwa au kuchukiwa vinawasilishwa kwenye mazungumzo kwa asilimia 38. Lakini maana zisizoelezwa kwa maneno ni asilimia 55 na asilimia saba, ndiyo yale maneno ambayo sisi sote huongea na kujifanya ndio uhalisia wenyewe.

Tuko kwenye siku 16 za uanaharakati kupinga ukatili wa kijinsia lakini yako mambo yamejitokeza mengi, ikiwamo hoja ya kutaka kuanzishwa Mahakama Maalum itakayokuwa na jukumu la kushughulikia kesi pekee zinazohusu ukatili wa kijinsia.

Lakini pia limejitokeza suala la watoto wengi wa umri wa kwenda day care (vituo vya kutwa vya kulea watoto) kufanyiwa ukatili kwa sababu unakuta wazazi wanakimbizana na kazi za ofisini ili wasifuikuzwe kwenye vibarua vyao.

Ni wajibu wa serikali, kuifumua Sheria ya Ajira na Uhusiano Kazini, Sura 366, ili kuongeza muda wa kumwezesha mama kukaa nyumbani hata kwa miezi sita, badala ya siku 84.

Ni vyema familia zichukue nafasi katika makuzi na malezi sahihi ya watoto. Tunaamini kwamba familia inayofanya parentive care, kuanzia walivyompata mtoto mpaka umri wa mtoto kujitambua, inasaidia sana kuotesha mbegu na maadili yatakayomsaidia mtoto katika kukua na kuondokana na suala zima la ukatili unaotokea ndani ya jamii.

Kwa hiyo, wazazi waache kazi nyingi ambazo zinawakimbiza huku na kule za kutafuta kipato. Wajue kwamba wana jukumu la msingi la kulea watoto kwa sababu suala la kulea watoto ni la msingi.

Watoto umewaleta duniani hawakuomba, umewaleta ukiwa na nia na makusudi ya kuwaweka waendelee kuishi vizuri. Ni vizuri pia kutenga muda mkubwa sana wa kuangalia majukumu ya walezi ya kulea hawa watoto.

Tunaona sasa hivi matukio pia ya ukatili wa kingono yanatokea sana hasa katika ngazi za familia. Hii inatokana na wale wamama, wadada wanaopata watoto katika umri ambao bado hawana nguvu za kufanya kazi za kiuchumi.

Kuhusu mahakama maalum za kushughulikia kesi za ukatili, mwanaharakati na Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Maendeleo la TUSONGE CDO, Aginatha Rutazaa, anasema kesi hizo kwa sasa zinashughulikiwa katika mahakama za kawaida na mara nyingi hazipati ule uzito wake wa kufanyiwa kazi kwa haraka, kwa ajili ya kusaidia wale waathirika waliofanyiwa matukio hayo.

"Tunajua kesi hizi zinashughulikiwa katika mahakama za kawaida na mara nyingi hazipati ule uzito wake wa kufanyiwa kazi kwa haraka kwa ajili ya kusaidia wale wahanga waliofanyiwa matukio haya.

"Kwa hiyo tunatamani sana kuishawishi na kuendelea kungana na wanaharakati wengine duniani kuomba serikali ya Tanzania, tukiihimiza tuweze kuwa na mahakama maalum, itakayokuwa inashughulikia tu masuala ya ukatili wa kijinsia," anasema.

Anasema wanatamani pia mifumo ile ya kisheria inayohusika na utatauzi, iangalie suala zima la ukatili wa kijinsia.

"Tuiombe jamii iache kutumia ile mifumo ya kijamii au ile ya mila ambayo inazidi kuendelea kukuza usawa na kupinga ukatili wa kijinsia ndani ya jamii. Kwa mfano kukaa kwenye ukoo, kujadiliana wazazi, ndugu, walezi mnaacha mhanga aliyefanyiwa tukio lile bila kujua mustakabali wa haki zake zikoje.

"Kwenye jamii mfano ya mkoa wa Kilimanjaro, kuna suala zima la kutumia masale, lile jani la amani ambalo pia wazazi wanakuja nalo kama alama ya kuomba msamaha baada ya mtu kufanyiwa tukio kubwa na lenye majeraha makubwa katika maisha yake," anasisitiza.

"Kwa hiyo tunatamani kwamba jamii nayo ichukue jukumu la kutumia ile mifumo sahihi ya kuripoti matukio ya ukatili ambayo ni mifumo ya kisheria, ili sheria zile zilizowekwa zichukue hatua na zichukue mkondo wake," anaongeza.

- ***Godfrey Mushi ni Mwandishi Mwandamizi wa Nipashe, Kanda ya Kaskazini. Anapatikana kwa simu namba 0715 545 490 au barua pepe: ghandsome79@gmail.com***

# HARUSI





Ilikuwa siku ya furaha kwa Frorah Nkunda wakati alipofanyiwa sherehe ya kipekee ya kuagwa kabla ya kufunga ndoa na mume wake Paul Kwayu jijini Dar es Salaam hivi karibuni. PICHA: MC GaraB.




MITINDO











# Tamba na Mama Samia

SUTI anayovaa Rais Samia Suluhu Hassan, maarufu kama Suti ya Mama Samia ni moja ya vazi linalozidi kupendwa nchini huku likipigiwa chapuo na wasanii na watu maarufu ambao wamejitokeza wakiwa wamevaa.

Hivi karibuni kumekuwa na kampeni ya kulitangaza vazi hilo, huku wasanii mbalimbali wanawake wakionekana wamevaa suti hiyo ikiwa na rangi tofauti.


Suti ya Mama Samia ambayo imetengenezwa kwa koti refu lenye vifungo mbele na kuambatana na suruali ndefu ni mtindo unaohifadhi heshima, unaovutia na wa kipekee pale mtu anapovaa kwa ajili ya shughuli mbalimbali.

Kupata umaarufu wa vazi hilo, linaleta shauku kwa wanawake wengi kwenda kununua au kushona ili angalau kuwa miongoni mwa wanaovaa.

Kimsingi suti hiyo inatumia vitambaa vya aina mbalimbali kama vitenge, Hariri, Khaki au Bazee na ni chaguo la mtu husika kitambaa gani anachopenda.

UREMBO

Na Mary Geofrey



# Makunyanzi sio tatizo ukifuata njia hizi za asili

MIKUNJO au makunyanzi yanatokana na kudhoofika kwa ngozi ni miongoni mwa matatizo yanayowakabili wanawake wengi.

Tofauti na mikunjo ya uzee, makunyanzi hutokana na kuchoka kwa ngozi kunakosababishwa na mambo mbalimbali.

Katika kupambana na tatizo hilo, wadau wa urembo wa asili wamegundua njia mbalimbali zinazoweza kutumika kutatua tatizo hili.



**Karoti**

Tumia juisi ya karoti kwa kupaka katika ngozi yako, hasa katika maeneo yaliyoathirika.

Karoti ina virutubisho muhimu kwa ngozi yako. Pia ina uwezo mkubwa wa kuondoa sumu ndani ya ngozi. Si hivyo tu, karoti inaweza kuondoa kabisa tatizo la mikunjo ya ngozi hasa sehemu za pembeni ya macho, shingo na maeneo kama hayo.



**Namna ya kufanya**

Chukua karoti, saga kwenye mashine kisha kamua ili kupata juisi yake.

Tumia pamba kupaka katika maeneo yaliyoathirika, fanya hivyo mara kwa mara, itakusaidia kupunguza ama kuondoa kabisa tatizo hilo.

**Maziwa**

Maziwa yana virutubisho vinavyochochea kunawiri kwa ngozi. Pia yana chembechembe za 'Alfa-Hydroxide Acid' ambazo zina uwezo mkubwa kuondoa seli zilizokufa mwilini.

Yote haya husaidia kwa kiasi kikubwa kuondoa tatizo la mikunjo katika ngozi.

**Namna ya kufanya**

Kuchukua maziwa kiasi na chovya pamba ndani yake, kisha paka maeneo yaliyoathirika.


MAPISHI

# Juisi ya maganda ya nanasi

UTAMU wa tunda la nanasi unajifaidi kwa kunywa kama juisi au kula lenyewe, lakini watu husahau kuwa maganda yake yana faida nyingi.

Watu hawafahamu kama maganda ya nanasi yana faida lukuki mwilini na yana ladha ya kipekee.

Maganda ya nanasi yanaweza kutoa juisi tamu pengine hata kulizidi tunda la nanasi lenyewe.



**Mahitaji**

Maganda ya nanasi kiasi cha juisi unayotaka, sukari kutokana na kiwango cha juisi na unavyopendelea, maji safi na sufuria itakayoweza kuhifadhi kiwango cha juisi utakayotengeneza, jiko, chujio, tangawizi na ndimu au limao.

**Maandalizi**

Osha maganda ya nanasi na tangawizi kwa maji safi kisha katakata na uweke kwenye sufuria tayari kwa kuchemsha.

Washa jiko, bandika sufuria yenye maganda ya nanasi na tangawizi. Weka maji kiasi chako kutokana na wingi wa maganda ya nanasi kwenye sufuria kisha ufunike uache ichemke kwa dakika 30 hadi maji yatakapobadilika na kuwa na rangi ya njano.

Maandalizi ya juisi hii ni rahisi hayahitaji blenda inayotumika wakati wa kusaga aina nyingine za juisi, hivyo hata kama umeme umekatika bado unaweza kutengeneza juisi hii na kufurahia pamoja na uwapendao.

Ikichemka hadi kiwango unachohitaji ipua juisi yako na uache ipoe vema. Baada ya hapo ichuje na uweke kwenye jagi, ongeza maji ya limao au ndimu na sukari na tayari kwa ajili ya kunywa.

## MAISHA NI NYUMBA

Na Restuta James

# Teknolojia inatosha kunogesha nyumba

TEKNOLOJIA imesaidia mageuzi katika utengenezaji wa samani, kuanzia muundo hadi umaliziaji (finishing), kiasi kwamba hakuna kitu kinachotengenezwa nchi yoyote kisichopatikana hapa nchini.

Hayo ni maneno ya fundi seremala, Ismail Mchambe, anayefurahia ulimwengu wa dijitali, unavyowarahisishia mafundi kubuni kazi mbalimbali za sanaa.

"Uzuri ni kwamba mteja akija na picha ya kiti, meza, kabati au chochote anachotaka, sisi tunakitengeneza. Tunazo samani za nyumbani, ofisini, shuleni, za nje na ndani. Ubunifu unakwenda kasi na sisi tunajitahidi hivyo hivyo," anasema.

Mchambe anasema amekuwa akibuni samani kwa kutumia mbao ngumu, japokuwa hivi sasa matumizi ya mbao laini yameongezeka.

Anasema kinachotofautisha samani za ndani na zile za nje, ni ubora wa mbao ngumu ikilinganishwa na mbao laini zinazotumiwa na mafundi wa nje ya nchi.

Anasema matumizi ya mashine za kisasa unafanya ukamilishaji mzuri wa samani na kwamba kwa mafundi wa nje, mashine zinawapunguzia matumizi ya mbao.

"Sisi bado tunatumia mbao nyingi ndio maana samani zetu ni bora japokuwa mwonekano unaweza usiwe mzuri sana. Za nje mwonekano ni mzuri, ubora ndio changamoto. Sisi tunaona kwamba badala ya kuagiza samani nje, tutafute sample tuwatumie mafundi wa ndani kuzitengeneza kwa mbao ngumu," anafafanua.



Na Elizabeth Zaya



# Nyumba yako inaonekanaje msimu wa sikukuu?

NI msimu wa sikukuu, kipindi ambacho kinakuwa na pilikapilika za hapa na pale katika nyumba, kukiwa kunaonekana kutawala mapambo yanayoshabihiana na msimu wenyewe.

Katika ofisi na sehemu mbalimbali ukipita au kuingia, unakutana na mapambo ya sikukuu, ukiwamo mti wa Krismasi ukiwa ndio umetawala.

Katika makala hii ya nyumba, tunakupa dondoo kidogo kukuongezea baadhi ya vitu ambavyo vitachagiza msimu wako wa mwaka huu kuwa mzuri zaidi na ukaufurahia ukiwa nyumbani kwako.

Naamini kwamba katika kipindi hiki, familia nyingi huwa zinaungana katika mapumziko ya mwisho wa mwaka, hivyo ni muhimu kukifanya kipindi hiki kikawa cha furaha zaidi kwa mapambo tofauti ya sikukuu ndani ya nyumba.

Mbali na mti wa Krismasi, pia yako mapambo mengine tofauti. Kama hutoweza kupata mti, unaweza pia kutafuta aina nyingine ya mapambo ambayo huenda yasikugharimu kabisa au ukayapata kwa gharama kidogo.

Lengo ni kuhakikisha nyumba yako inachangamka na kuipa raha familia ambayo imekusanyika nyumbani kwa ajili ya mapumziko ya mwisho wa mwaka.







Unaweza kuchanganya na mapambo mengine tofauti kama 'wall papers' na maua mengine kwa kuzingatia rangi zinazoshabihiana na msimu wenyewe.

Kwa mfano, mapambo mengine ambayo yanaweza kutumika Krismasi ni pamoja na karatasi za rangi, taa za kung'aa, mapambo ya karatasi yanayotengenezwa kwa mtindo wa nyota.

Mengine ni kengele za Krismasi, picha za kondoo, farasi, mipira ya kung`aa, wanyama wadogo wa kutengenezwa kama kondoo.

Mapambo mengine ambayo unaweza kutengeneza ni ya maua ya asili kwa kuyaweka katika chombo au chupa maalumu ambacho kinaweza kuwekwa hata juu ya meza.

Pamoja na kupendezesha nyumba, pia hewa na harufu hubadilika na kuwa nzuri zaidi kutokana na maua yanayowekwa ndani.


Unaweza kupamba pia maneno yenye ujumbe maalum ambayo unaweza kuyaandika mwenyewe ya kuendana na msimu au ukayanunua katika sehemu maalumu yanapopatikana.

Hakikisha unaweka mapambo sehemu ambayo ni salama na hayawezi kuharibika kwa namna yoyote au kuharibiwa na watoto.

Pia nyumba katika musimu huu inatakiwa iwe inapigwa nyimbo zinazoshabihiana na msimu wenyewe.

Baada ya kuisha kwa msimu unatakiwa uyaondoe na kudizaini upya muonekano wa nyumba yako.

## KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2024
SMS - 0713 447766
JUKWAANI
NIMEGOMBEA KWA 'TIKETI' YA CHAMA KUBWA HOLA!...NIKARUDIA KWA 'TIKETI' YA UPANDE WA PILI NIKALA MWELEKA! SASA NAGOMBEA KWA 'TIKETI YA TRENI' NIONE
HII MIPOMBE YA KUJIANGUSHA HOVYO HOVYO MBELE YA MASELA USIDHANI SIFA KITAKUKUTA KITU CHA KIHISTORIA
ACHANA NA MIMI NAKULA TIZI' LA KWENDA MOSHI KRISIMASI KWANI WE HUJUI?
USWAZI RAHA SANA! USIKU JITU LINAKULA 'MAKONDE NA MKEWE' ASUBUHI TUNALICHORA TUNALIONA KATUNI
USWAZI SH'KAMOO!
SIJALAZIMISHWA NA MTU NIKIWA NA AKILI TIMAMU BILA KUVUTA 'BANGE' NAACHA KAZI LEO
KAMA MKEO NDIO AMEKUSHAURI NASEMA SKUBALI NNA UPATU, NNA VIKOBA KILA SEHEMU NASEMA SIKUBALI
MAOMBI NI BALAA! WATEJA WOTE WAME-HAMIA HUKO WAMENIACHA MKIWA, SASA NA MIMI NATAFUTA SUTI KALI SANA NAHAMIA KWENYE UNABII KULALEKI...@!

# Viongozi duniani washiriki uzinduzi kanisa kongwe

**PARIS,** UFARANSA

VIONGOZI mbalimbali duniani, akiwamo rais mteule wa Marekani, Donald Trump, wamehudhuria sherehe za kufunguliwa rasmi Kanisa Kuu la Notre-Dame la mjini Paris.

Rais wa Ufaransa Emmanuel Macron, aliwaalika viongozi 50 kutoka pande zote za Dunia kushiriki ufunguzi wa kanisa hilo ambalo lilichomwa moto wakati wa moto mkubwa mwaka 2019.

Kanisa hilo ambalo liko katikati ya mji mkuu wa Paris, limekuwa nembo ya taifa na kivutio kwa watalii wanaotembelea nchi hiyo.

Viongozi wengine waliohudhuria tukio hilo ni pamoja na Rais wa Ujerumani Frank-Walter Steinmeier, Rais wa Kamisheni ya Ulaya Ursula von der Leyen na Rais wa Italia Sergio Mattarella.

Trump alitangaza kuhudhuria tukio hilo siku chache zilizopita kwenye mtandao wake wa kijamii wa Truth na kuwa safari yake ya kwanza nje ya Marekani tangu apate ushindi katika uchaguzi uliofanyika Novemba 5, mwaka huu.

**DW**

# Waasi Syria wachanja mbuga kumwangusha Rais Al Assad

**HAMA,** SYRIA

VIKOSI vya waasi nchini Syria, vimeripotiwa kuteka sehemu kubwa ya eneo la Deraa, ambalo lilikuwa chanzo cha maasi dhidi ya Rais Bashar Al-Assad mwaka 2011.

Wachunguzi wa vita wenye makao yake nchini Uingereza walisema vikundi vya ndani vya wapiganaji viliweza kuchukua udhibiti wa maeneo mengi ya kijeshi kufuatia mapigano makali na vikosi vya serikali.

Kulingana na shirika la habari la Reuters, vyanzo vya waasi vilisema kuwa wamefikia makubaliano na jeshi la serikali kuondoka na maofisa wa kijeshi ili wapewe njia salama kuelekea mji mkuu, Damascus, ambao uko umbali wa kilomita 100.

Hata hivyo, hakuna uthibitisho kutoka chanzo huru kuhusu taarifa hizo.

Waasi hao wanaoongozwa na Waislamu kutoka kaskazini mwa Syria, wanadai kufika viunga vya mji wa Homs.

Katika hatua nyingine, sanamu la mwanzilishi wa taifa hilo marehemu Hafez al-Assad, ambaye ni baba yake Rais Bashar al-Assad, ambayo iliwekwa katika mji wa Homs iliangushwa jana na waasi hao.

Katika taarifa ya waasi hao ilisema wamechukua udhibiti kamili katika mji huo wa pili kwa ukubwa nchi humo, baada ya jeshi kuondoka.

Kiongozi wa kundi la wanamgambo wa Kiislamu Hayat Tahrir al-Sham (HTS), Abu Mohammed al-Jawlani, alitangaza ushindi jana akiwa katika mji wa Hama na kueleza hakutakuwa na kisasi.

Hapo awali, wapiganaji wa HTS na washirika wao waliliteka gereza kuu la Hama na kuwaachilia wafungwa wakati kukiwa na vita vikali, Jeshi la Syria lilisema kuwa liliwarudisha nyuma wanajeshi wake nje ya mji huo.

Hama ni makazi ya watu milioni moja na iko kilomita 110 kusini mwa jiji la Aleppo, ambalo waasi waliliteka wiki iliyopita baada ya kufanya mashambulizi ya kushtukiza kutoka ngome yao kaskazini-magharibi.

**BBC**



Kifaru cha jeshi la serikali kikiwa kimetelekezwa katika barabara inayoelekea mji mkuu wa Syria wa Damascus juzi. **PICHA: Reuters**

# Wabunge waondoka bungeni, kumlinda Rais kung'olewa

**SEOUL,** KOREA KUSINI

WABUNGE wa chama tawala cha Korea Kusini cha People Power Party (PPP), wameondoka ndani ya bunge, kabla ya kufanyika upigaji kura ya kumuondoa madarakani Rais wa nchi hiyo, Yoon Suk Yeol.

Kundi la wabunge 107 kati ya 108 wa chama tawala, waliondoka bungeni na kusababisha kuwepo kizaazaa cha baadhi ya wabunge wa upinzani kutaka kuwazuia.

Hata hivyo, wabunge waliobaki ndani ya bunge waliendelea na taratibu za kumuondoa madarakani Rais Yoon Suk.

Huenda wawakilishi wa chama hicho walitumia mkakati huo wa kususia upigaji kura ili kuzuia watu kuasi, kwani kura ya kumuondoa hupatikana kwa upigaji wa kura za siri.

Ahn Cheol-soo, profesa aliyegeuka kuwa mwanasiasa ambaye aliwania urais mwaka wa 2012, 2017 na 2022, ndiye mbunge pekee wa PPP ambaye amebaki katika kiti chake.

Ahn amekuwa akisema mara kwa mara kuwa atapiga kura ya kufunguliwa mashtaka ikiwa rais hatajiuzulu kwa hiari kabla ya upigaji kura.

Wabunge wengi wa vyama vya upinzani wamekusanyika bungeni wakijaribu kukimbilia mlangoni wakati wabunge wa chama tawala walipoanza kuondoka, wakijaribu kuwazuia. Wakati wa pilikapilika hizo, wabunge wa upinzani walikuwa wakiimba "wasaliti" na "rudi tena kupiga kura".

Mwandishi wa BBC alisema ndani ya bunge kulikuwa na hasira kutokana na mwanachama mmoja tu au wawili wa chama tawala ambao bado wamesalia ndani ya ukumbi.

Nje ya bunge, kulikuwa na umati wa watu huku Wakorea wengi zaidi wakikusanyika kwenye barabara ya bunge, huku polisi wakiimarisha ulinzi. Maandamano hayo yalikuwa yakifanyika karibu na kituo cha treni ya chini ya ardhi, waandamanaji wakiweka vizuizi kuzuia treni.

Mamlaka iliamua kufunga kituo hicho, na polisi wamepanga mistari kwenye maeneo mbalimbali kuongoza umati wa watu wanaoandamana.

Wakati huo huo, Rais Yoon Suk, ameomba radhi kwa taifa lake kutokana na amri yake ya kutangaza sheria ya kijeshi, hatua ambayo ilizua ukosoaji kutoka kwa raia na mataifa ya nje.

Katika hotuba aliyoitoa muda mfupi kabla ya kikao cha bunge, Rais Yoon alisema anatambua kuwa uamuzi wake wa kutangaza sheria hiyo ulisababisha mtafaruku kwenye nchi na amewaomba raia wamsamehe.

Huku akiinamisha kichwa chake chini, rais Yoon alisema anakiachia chama chake kuamua hatima yake, ikiwa aendelee au aondoke madarakani.

Awali, mkuu wa chama kinachotawala, Han Dong-hoon, alisema kwamba kujiuzulu kwa rais huyo ni jambo lisiloepukika, kwani hana nafasi ya kutekeleza majukumu yake kwa umma.

**BBC**

HABARI/SAFU

# Othman awatwisha zigo wazee mmomonyoko maadili

Na Mwandishi Wetu

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman (pichani), amesema wananchi hasa wazee wana jukumu kubwa la kuitathmini jamii kutafuta mahali walipokosea na kurekebisha ili kuiokoa Zanzibar kuendelea kuharibika kimaadili.

Othman ambaye pia ni Mwenyekiti wa Taifa wa Chama cha ACT Wazalendo, ameyasema hayo juzi katika msikiti wa Ibadhi, Mtemani.

Wete kisiwani Pemba alipowasalimia waumini wa dini ya Kiislamu baada ya kuungana nao kukamilisha ibada ya swala ya Ijumaa.

Alisema jamii yote ya Zanzibar ina jukumu la kutekeleza katika kuhakikisha maadili katika kizazi kilichopo na kijacho yanalindwa na hayaporomoki, hivyo kuifanya Zanzibar kuendelea kubaki na sifa njema iliyopo kwa muda mrefu na kuheshimika sana duniani kote.

Taarifa iliyotolewa na Kitengo cha Mawasiliano Ofisi ya Makamu wa Kwnza wa Rais ilisema, Othman alibainisha kwamba hivi sasa jamii imejisahau na kudhani kwamba jukumu la malezi bora kwa watoto linapaswa kutekelezwa na viongozi wa serikali pekee. Alisema fikra hizo zinazaweza kuchangia kuongezeka kwa tatizo la maadili kuporomoka nchini.

Alisema katika miaka ya nyuma suala la malezi na kusaidia uongofu kwa mtoto halikufanywa na mzazi aliyemzaa mtoto pekee bali jamii yote ilihusika kwa kuamini kuwa jukumu hilo ni la wote na kwamba utaratibu huo u;lisaidia sana maadili kulindwa.

Pia aliwakumbusha waumini na wanajamii wote kwamba jambo linaloweza kuchagia hali hiyo ni watu kutokumwogopa Mwenyezi Mungu na kuhimiza kuwapo amani bila ya kuitetea haki ndani ya jamii kwa kuwa pasipo haki na amani pia hutoweka.



Alisema kutokana na hali hiyo, Wazanzibari wamekuwa wakitendeana maovu miongoni mwao na kutamani kupata zaidi hata kwa njia ya haramu jambo ambalo linaivunjia heshima kubwa ya kimaadili iliyokuwapo Zanzibar kwa muda mrefu.

Othman aliwataka wanajamii kujitahidi kwa pamoja kurejesha tabia njema Zanzibar ili kuifanya kubaki na sifa njema kama ilivyowahi kupigiwa mfano wa kuitwa Andalosi ya Afrika ambao mji maarufu sana ulioko Hispania unaosifika kwa kila sifa njema miaka kadhaa iliyopita hadi sasa.

Akitoa hotuba ya swala ya Ijumaa, Shehe Ali Issa Khamis wa Msikiti huo, aliikumbusha jamii na viongozi kujitahidi katika malezi ili kurejesha heshima ya Zanzibar kimaadili kwa kuwa hivi sasa maadili kwa kiasi kikubwa yanaporomoka.

Amekemea tabia ya wanawake na wasichana kuvaa nguo zisizositiri vyema miili yao kwa mujibu wa mwongozo wa dini ya Kiislamu na kuitaka jami kuhakikisha jambo hilo inalikemea kupitia malezi bora ya watoto wao.

Othman alitarajia jana kumaliza ziara yake ya wiki moja kisiwani Pemba iliyohusisha shughuli za chama na serikali na alitarajiwa kurejea Unguja baada ya kuhudhuria Kongamano la Ngome ya Wanawake wa ACT Wazalendo lililofanyika Chakechake.

# Wafanyabiashara kortini madai biashara dawa za kulevya

Na Grace Gurisha

MFANYABIASHARA Geofrey Barnabas (29) na wenzake wawili, wamepandishwa kizimbani wakikabiliwa na mashtaka ya kufanya biashara ya dawa ya kulevya aina ya codeine kilogramu 53.93 katika ofisi ya DHL zilizoko Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere.

Washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni mfanyabiashara Isaya Japhet (30) na mfanyabiashara Jovistus Butatondewe (27) wote wakazi wa Mongolandege, Dar es Salaam.

Wakili wa Serikali, Tumaini Mafuru, alidai juzi mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Gwantwa Mwankuga, kuwa washtakiwa wanakabiliwa na mashtaka mawili.

Alidai kuwa Barnabas, anashtakiwa kujihusisha na dawa za kulevya na kwamba Oktoba 9, mwaka huu, katika ofisi za DHL zilizoko JNIA, alikutwa akifanya biashara ya dawa za kulevya aina ya codeine kilogramu 14.52

Wakili Mafuru alidai kuwa shtaka la pili la kufanya biashara ya dawa za kulevya linalowakabili washtakiwa wote kwa pamoja.

Iliadaiwa kuwa katika tarehe hiyo hiyo eneo la Ukonga Mongolandege ndani ya wilaya, Ilala mkoani Dar es Salaam, kwa pamoja walikutwa wakifanya biashara ya dawa za kulevya aina ya Codeine kilogramu 39.41.

Hakimu Mwankuga alisema kutokana na aina ya shauri wanaloshtakiwa nalo washtakiwa hawatakiwi kujibu chochote.

Wakili Mafuru alida kuwa upelelezi wa kesi hiyo bado unaendelea na kuomba washtakiwa wasipewe dhamana kwa kuwa kiasi cha dawa wanachoshtakiwa nacho hakiruhusu dhamana kwa kuzingatia sheria.

Kesi hiyo iliahirisha hadi Disemba 17, mwaka huu, kwa ajili ya kutajwa.

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# *Visa, mikasa ya michepuko ya zamani*



Na Adam Fungamwango

HAKUNA kitu chochote kinachofanywa kwenye kizazi cha sasa ambacho huko nyuma hakikuwepo. Kizazi cha sasa kinanufaika zaidi na teknolojia tu ambayo imekuwa kubwa sana na kurahisisha kazi na vitu vingi, lakini kwenye maisha ya kawaida kwenye jamii kila kitu kilikuwepo na watu walifanya zaidi kuliko wa sasa.

Watu wenye akili walikuwepo tangu enzi hizo na ndiyo wengi wao ni wavumbuzi wa kila kitu, hata herufi hizi tunazotumia. Watu wenye roho mbaya unaowajua wewe hivi sasa hakuna kitu, kuna watu walikuwa na roho mbaya miaka hiyo ya nyuma kuliko sasa.

Ndipo kulikuwa na hukumu za kunyonga watu hadharani, kuwambwa kwenye miti na hata kuchomwa moto, adhabu ambazo kwenye ulimwengu wa sasa hazipo tena.

Dunia imestarabika sana, na sheria zinazowekwa sasa ni kwa sababu huko nyuma ilikuwa ni hatari sana. Mwenye nguvu aliweza kufanya vyovyote vile na asifanywe lolote.

Tunasikia eti kwa sasa watu wamebadilika, hasa wanaume wamekuwa na wanawake wengi nje, maarufu kama michepuko.

Inawezekana ikawa ni kweli, lakini ukiangalia sana unagundua kuwa hakuna kilichobadilika. Maisha ni yale yale tu. Hata zamani watu walikuwa na michepuko, si wanawake wala wanaume.

Hizi ni tabia za mtu binafsi, kwani kwenye maisha ya kawaida huwezi kukuta watu wanafanana tabia hata kama wamezaliwa baba na mama mmoja.

Wakati hata zamani kulikiwa na watu wenye tabia njema na waadilifu, lakini ambao hawakuwa waadilifu nao walikuwapo.

Ushahidi wa hili umo kwenye baadhi ya nyimbo ambazo tunaziangalia hapa. Kwa kawaida wanamuziki hasa wa zamani hutunga nyimbo kutokana na kile anachokiona kikifanyika, au kilichotokea ndani ya jamii. Na ndiyo maana wakaitwa kioo cha jamii.

Tuanze na wimbo wa 'Edita' uliotungwa na Hassan Rehani Bitchuka mwanzoni mwa miaka ya 1980.

"Kipenzi changu Edita sikia ukweli niliokuwa nao, kusema kweli nimechoka na tabia yako. Ni siku nyingi nimelezwa mengi niliopuuza, nilijua ni fitina za majirani tu, wanataka kututenganisha. Lakini leo nimeamini, kipenzi Edita, methali ya kiswahili yasema kwamba lisemwalo lipo. Nikitoka kazini sikukuti, nikuulizapo ulikuwa wapi? Nilikuwa kwa shangazi Kariakoo, kumbe una wako wa pembeni, kipenzi Edita. Hukuridhika mpaka umemleta kwako, wakati sipo niko kazini, waweza kuchukua kila chako, uende zako, kipenzi Edita."

Wimbo ni ushaidi tosha kwamba haya mambo yalikuwepo enzi na enzi na si kusema eti kizazi hiki cha sasa kimezidi.

Kama dunia inaendelea na watu wanazidi kuzaliwa, na kizazi kinakuja, kinaondoka na kuja kingine, haya yataendelea tu kwa sababu maisha ni mzunguko.

Hicho ni kisa cha mwanamke aliyekuwa akimzunguka mume wake na kumleta mchepuko wake ndani. Ni hatari sana na inaumiza.

"Kila siku mke wangu unarudi saa za usiku ufikapo nyumbani macho yau yau, nimevumilia sasa nimechoka, leo nataka unieleze ukweli, wapi unapochelewa.

Nachelewa stendi ya basi bwana ee, tabu ya mabasi waijua mume wangu, nihurumie bwana."

Wimbo huu unaitwa 'Stendi ya Basi' ulitungwa na Adam Bakari katikati ya miaka ya 1980 akiwa na Orchetra Tomatoma. Mke anachelewa kurudi nyumbani, mumewe akimuuliza anamwambia kachelewa stendi ya basi.

Hapa tunaona hata uongo nao unakwenda na wakati. Zamani kulikuwa na shida ya mabasi, akatumia uongo huo. Hivi sasa asingeeleweka. Mabasi yako mengi tu tena wanakaa mpaka foleni kusubiri abiria. Dada kwa sasa angesema kulikuwa na foleni ya magari. Uongo lazima uendane pia na wakati.

Huyu alikuwa anachelewa kwa mchepuko wake, halafu anakuja 'kumfunga kamba' mumewe. Hemed Maneti naye katikati ya miaka ya 1970 akiwa na Vijana Jazz, alitunga wimbo unaitwa 'Niliruka Ukuta'.

Jamaa ana mke, akakutana na mwanamke ambaye naye ana mume lakini amesafiri. Hapo kila mtu akawa mchepuko wa mwenzake. Mwanamke akamdanganya mwanaume kama hajaolewa, hivyo akaenda kwake. Kilichomkuta huko ni hatari tu.

"Nenda upesi nenda kamwambie, tokea leo asinifuatefuate, kitendo alichonitenda, kingenifanya nipoteze maisha. Kuniambia kwamba hajaolewa, na kile chumba amekipanga yeye, kumbe uongo amenidanganya, ikipofika saa nane ya usiku, nikasikia hodohodi fungua, bahati nzuri, kikaruka ukuta.

"Kama ukifika mwambie ajirekebishe, mambo kama yale mabaya na yana hatari. Kusema kweli si vibaya na wala dhambi, ya nini sasa kunificha na kunidanganya. Maisha yangu yangekwisha sababu ya yeye. Nimeponea chupuchupu nashukuru Mungu, kama si kuruka ukuta ingekuwa hatari."

Wimbo huu unaonyesha hasara ya michepuko, unaweza kudanganywa na kuingia mkenge, hivyo kuwa makini au salama zaidi ni 'kubaki njia kuu.'

**Tuma Meseji 0716 350534**

# HADITHI

## Nyuma ya Pazia-12

TAARIFA za habari kwenye televisheni, redio, mitandao ya kijamii zinaarifu kutekwa kwa mtoto wa miaka sita, Macaire, mwanafunzi wa darasa la kwanza katika shule moja Mbezi Dar es Salaam. Mashuhuda wanasema alinyakuliwa na mwanamume mmoja aliyeshiba, kujaa misuli na kukimbilia kwenye gari lililokuwa pembeni mwa barabara ya Bagamoyo, Dar es salaam, ambalo mlango wake ulikuwa wazi. Wazazi wa mtoto wanapigiwa simu na watekaji wakitaka kiasi cha Sh. Milioni 15 ili wamwachie. Jeshi la Polisi linaingia kazini kumsaka au kuwasaka watekaji. Walichogundua ni kisa cha kushangaza, kusisimua ambacho utakipata utakaposoma kila aina ya nakala ya gazeti hili, ili kuupata mkasa mzima wa tukio.

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

SASA unasikia dada yangu, achana na hao askari, maana inaonekana kuna mtu anatoa anawapa taarifa, mimi nataka kukusaidia mtoto wako aachie huru. Nataka nikusaidie kiasi cha Sh. Milioni 15 ambazo nitazikopa kutoka kwa rafiki yangu." Macho yalimtoka pima Dora na kumuuliza Eddy,"unasema kweli?" "Ni kweli kabisa." "Mbona nitashukuru maana nina hamu na mwangu ndugu mwandishi."

Ilikuwa ni siku ya pili baada ya Eddy kuongea na baba wa mtoto aliyetekwa, na sasa alikuwa anaongea na mama yake mzazi.

Ikumbukwe wote wawili waliongea kwa nyakati tofauti na Eddy, bila kujua kuwa ni mpelelezi anayetaka kuwakamata waliomteka mtoto wao, lakini kujua ni kitu gani kinakwamisha wahusika watiwe mbaroni kwani wanaonekana wanajua kila kinachofanyika kutoka kwa maafande na wazazi.

"Hizi ni mimi mwenyewe nimeamua kukupa, nitazilipa mwenyewe taratibu.

Ninachotaka kufanya ni kwamba tukaweke sehemu ambayo wao wataamua ili mtoto wako apatikane arudi nyumbani. na Hili hatuishirikishi polisi.

Ni kwamba nataka watekaji wachukue pesa ili wamuachie mtoto na si mtego kama wanavyofanya polisi." Dora alionekana kupatwa mshagao asiamini anachokisikia. "Unasema kweli?" "Kweli bibie!"

"Mbona nitashukuru sana jamani, mtoto wangu sijamuona siku nyingi." Alisema na kuanza kulia.


Eddy alipata kazi ya dakika kama tano hivi ya kumbembeleza. Alipokaa sawa akamuuliza. "Enhe sasa tutajuaje kama watekaji hao ni lini watautaka mzigo huo kwa sababu anayepigiwa siku zote na kuamrishwa ni mzazi mwenzako tu?" Lilionekana ni swali muhimu mno kwa Dora.

"Sasa hapo!" Dora kachagiza. "Sasa tunafanyaje?" Eddy akamuuliza Halafu akauliza tena.

"Au tumshirikishe?" "Mhh sijui, wewe ndiyo mpanga plani. Mimi nafuatisha tu. Na hapa ni lazima tujue ni lini ameambiwa."

Eddy tayari alishaambiwa na Macky kuwa ni kesho kutwa. Lakini hakutaka kabisa kumwambia Dora. Nia ni ile ile.

Kuwatenganisha. Tayari alikuwa amewatenganisha askari polisi na sakata hili. Hapa sasa alikuwa anawatenganisha Macky na mzazi mwenzake Dora.




**Mpaka hapo alikuwa amefaulu, kwani aliongea na Macky kama mwandishi wa habari. Na tayari alishamwambia atamkopesa kiasi cha Sh. Miliono 15 kutoka kwa rafiki yake kwa ajili ya kumkomboa mtoto.**

Nia ni ile ile kutaka kujua kwa nini siri inatoka? Nani atatoa siri? Pia kuwanasa watuhumiwa.

Mpaka hapo alikuwa amefaulu, kwani aliongea na Macky kama mwandishi wa habari. Na tayari alishamwambia atamkopesa kiasi cha Sh. Miliono 15 kutoka kwa rafiki yake kwa ajili ya kumkomboa mtoto. Hakutaka kumuunganisha na mzazi mwenzake Dora.

Kwa upande wa Dora naye alitambua kama Eddy ni mwandishi wa habari. Yeye aliambia atasaidiwa kwa asilimia 100 kupewa kiasi hicho cha ajili ya kumkomboa mtoto.

Kwa maana hiyo, Macky na Dora kila mmoja alijua ameongea peke yake na mwandishi huyo, na kila mmoja akaambiwa asimwambie mwenzake ili kulinda usiri.

"Mimi nina wazo!" Alisema Eddy baada ya kuwaza kwa dakika kadhaa. "Mimi simjui huyo mzazi mwenzako na sitaki tumuunganishe kwa hili. Ila unaweza kufanya kazi moja ukafanikiwa." "Kazi gani?" Akauliza huku akitabasamu. "Wewe ni mtoto wa kike. Nikisema hivyo unajua.

Yule ni mzazi mwenzako. Unaweza kumshawishi ili kujua siku na wapi hiyo pesa watekaji wanataka iende ikawekwe sawa?" Dora alitulia kidogo kama anafikiri kitu, halafu akasema. "Nitajaribu."

"Ninavyojua mwanamke akitaka jambo lake hakuna anayeweza kumzuia.

Tunachotaka sisi kujua tu lini ni wapi ameambiwa akaweke hizo pesa, halafu uje kwangu ili sisi ndiyo tukaweke hizo pesa kwa sababu yeye siku zote pesa zake ni za mtego wa polisi, sisi tutakwenda kuweka mapema zaidi kuliko yeye ili wazichukue kabla za mtego hazijaja. Nadhani tunaelewana hapa."

"Nimekuelewa baba. Nitafanya kila linalowezekana kwa ajili ya mtoto wangu, Macaire," alisema Dora.

Eddy alisema hivyo wakati alimwambia Macky asitoe siri hiyo kwa mtu yoyote, si askari polisi wala mzazi mwenzake Dora. Hapo tayari alikuwa ameshauweka mtego. Nani atatoa au kuvujisha siri.

Ameongea na wote wawili kila mmoja kivyake. Je maneno ya upande huu yatavuja upande wa pili?

**************************************

Ilikuwa saa 10 jioni Eddy aliposikia moja kati ya simu zake za mkononi zikilia.

Ni ile ambao namba yake alimpa Dora, mama wa mtoto Macaire aliyetekwa.

Alikuwa anajiandaa kutoa ofisini. Alitoa namba hiyo ili kama akifanikiwa mpango waliopanga. "Enhee niambie shemeji." Eddy akadakia. "Bwana we, ile ishu yetu hatimaye imefanikiwa!" Eddy akenua meno. Akataka kucheka, lakini hakuwa na kicheko chochote wala sababu ya kufanya hivyo.

"Imekuwaje rahisi kiasi hiki shemeji, kweli we siyo mtu mzuri!" "Si ulisema mwenyewe wanawake hatushindwi kitu. Nimefanikiwa nilipotoka saa nne asubuhi ofisini kwako, nilijaribu kuwasilia naye. Akawa anapingapinga..." "Shemeji, naomba usiendelee kuongea kwenye simu, kuna masikio ya watu humu, nataka leo hii hii uje ofisini kwake tupange mipango.

Nitakutumia pesa sasa hivi ili akodishe gari kwa njia ya mtandao ufika hapa mara moja kwa ajili ya mazungumzo uniambie ilikuwaje hadi mambo yameenda vizuri hivi, lini, wapi na saa ngapi."

"Sawa shemeji." Eddy alijua kabisa kama Dora amejua ni sehemu ambayo matekaji wanataka pesa ipelekwe, basi Macky amevujisha siri kwa mzazi mwenzake. Kwa maana hiyo amekiuka makubaliao baina yake kuwa asimwambie mtu yoyote.

Masaa mawili baadaye Dora aliingia ofisini kwa Eddy. "Habari yako shemeji." Akamsalimia kwa tabasamu.

Tayari Dora alionekana kumzoea Eddy. Na hii ni kwa sababu mpelelezi huyo ni mtu wa utani na kuzoeleka kwa urahisi. Pia hakujua kama ni mpelelezi, ila mwandishi wa habari, kazi ambayo ndiyo alijitambulisha nayo.

"Nipe habari shemeji. Nadhani umefanya kazi nzuri." "We acha tu, haikuwa rahisi ndugu yangu, mbishi yule baba!" "Enhe ulipofika ulimfanya nini hadi akakubali na amesema kama amesiliana na watekaji?" Akauliza na kumuacha kwanza akae kwenye kochi la ofisini.

"Mwenzako nilipotoka hapa nikampigia simu tukutane kwa ajili ya kutafakari jamabo hili kwa sababu mtoto ni wangu mimi na yeye. Akawa mgumu, lakini nimemdanganya kuwa nina wazo ambalo linaweza kusababisha mtoto apatikane kwa haraka.

Akaniuliza tukutane wapi, maana kwake hataki, mchumba wake anaweza kufika muda wowote.

Nikamwambia tukutane faragha, kwenye hoteli yoyote kwa sababu wote wawili tuna mahusiano, hakuna yoyote anayetaka kuyavunja.

Akaniambia niende kwenye hoteli ya Malimba kule Sinza. Nikaenda tukakutana.

Ilikuwa ndani tukaongea, Nikamdanganya. Mimi mtoto wa kike bwana, nikamlegeza pale akalegea mwenyewe. Akaingia laini. Baada ya kumaliza nikamuuliza, enhee walikupigia simu watekaji, wanasemaje? Na wapi safari hii?"

**Itaendelea Jumapili**



# ROMA AAMUA KUGEUKIA UALIMU

RAPA mwenye utata, Roma Mkatoliki, hatimaye amewageuka kuwa mwalimu wa ujasiriamali na kuwahamasisha vijana kutengeneza pesa.

Roma amesema katika maisha kuwa tajiri ni jambo rahisi kama utaweza kuchagua biashara na kupanga mapato na matumizi kwa usahihi.


Kupitia ukuyrasa wake wa Instagram, msanii huyo amesema kwamba uthubutu ni jambo linalotakiwa katika kuanza kwa kila biashara.

# *Monalisa kawa mwigizaji msomi*

MWIGIZAJI mkongwe wa filamu za Bongo Muvi, Monalisa, amewajibu kwa vitendo watu waliokuwa wakisema ameisha kisanaa, akisema kwa sasa amekuwa msomi wa biashara baada ya kuhitimu masomo ya chuo kikuu.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, Monalisa amesema kuna watu walikuwa wakimbeza kwa hatua yake ya kwenda kusoma, kutokana na uvumilivu wake amepata cheti na kuwa mwanafunzi bora katika fani ya biashara na usimamizi wa miradi.

“Walisema nimeshazeeka kwanini nirudi shule? Kufanya nini? Na wengine walinicheka sana kuniona naingia darasani na hawakuamini kwenye dhana ya kuanza upya. Huu ni ushuhuda wa uvumillivu, ujasiri na uthubutu” ameandika Monalisa.



## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

#### MADRID YAMTAKA DALOT

REAL Madrid imewasiliana na beki wa Ureno, Diogo Dalot mwenye umri wa miaka 25 na wameambiwa Manchester United inataka pauni milioni 41.5. Hata hivyo, beki wa Liverpool na England, Trent Alexander-Arnold mwenye umri wa miaka 26, atabakia kuwa kipaumbele cha mabingwa hao wa Hispania. ***(Relevo)***

#### SALAH YUPO TAYARI KUBAKI

WINGA wa Misri, Mohamed Salah yuko tayari kusaini mkataba mpya wa mwaka mmoja katika klabu ya Liverpool lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32 anazidi kukasirishwa na jinsi klabu hiyo inavyoshughulikia mazungumzo. ***(Athletic)***

#### CONCEICAO AWANIWA EPL

KLABU ya West Ham inamfikiria kocha wa Porto, Sergio Conceicao kuchukua nafasi ya Julen Lopetegui, ambaye mustakabali wake kama kocha unakabiliwa na shinikizo kubwa. ***(Guardian)***

#### DIALLO KUSAINI MAN UNITED

KOCHA wa Manchester United, Ruben Amorim anatazamiwa kufanya mazungumzo kuhusu mkataba mpya na winga wa Ivory Coast, Amad Diallo mwenye umri wa miaka 22, ambaye mkataba wake unakamilika msimu wa majira ya joto. ***(Telegraph)***

#### SANE KUPEWA MKATABA

KLABU ya Bayern Munich imeanza mazungumzo ya kuongeza mkataba wa winga wa Ujerumani, Leroy Sane mwenye umri wa miaka 28. ***(Sky Germany)***

#### KUSITISHIWA MKATABA

KLABU ya Leicester City inafikiria kusitisha mkataba wa mkopo wa msimu mzima wa mshambuliaji wa Crystal Palace, Odsonne Edouard mwenye umri wa miaka 26 Januari. ***(Football Insider)***

#### MAMBO MAZURI MADRID

REAL Madrid wanapanga kumpa beki wa Hispania, Raul Asencio mkataba mpya wenye masharti bora zaidi. ***(Fabrizio Romano)***

#### ASTON VILLA KUSAKA BEKI

KLABU ya Aston Villa italenga beki mpya wa kulia kwenye dirisha la usajili la Januari. ***(Football Insider)***

#### EDERSON AGOMBEWA EPL

KLABU za Manchester United, Manchester City na Liverpool zote zinamtaka kiungo wa kati wa Atalanta na Brazil, Ederson, lakini itahitaji ofa kubwa kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25. ***(TeamTalks)***

#### KIWIOR KUONDOKA ARSENAL

FIORENTINA na Napoli zinatazamia mkataba wa mkopo kwa mlinzi wa Arsenal, Jakub Kiwior lakini kuna uwezekano kocha Mikel Arteta atamruhusu mchezaji huyo wa kimataifa wa Poland mwenye umri wa miaka 24 kuondoka Januari. ***(Tuttomercato)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# PSG HAINA MPANGO NA MOHAMED SALAH

**PARIS,** Ufaransa

**Rais wa timu hiyo licha ya kuweka wazi mapenzi yake kwa nyota huyo, amesema...**

RAIS wa klabu ya PSG, Nasser Al-Khelaifi amesema "anampenda" winga wa Liverpool, Mohamed Salah lakini akabainisha kwamba hakuna ukweli wowote kuhusu uvumi unaomhusisha na uhamisho wa kujiunga na wababe hao wa Ufaransa.

**Mustakabali wa Salah ndani ya Anfield bado haujulikani huku mkataba wake wa sasa ukitarajiwa kumalizika mwishoni mwa msimu huu.**

Mmisri huyo ana mabao 21 kwenye Ligi Kuu hadi sasa msimu huu, sita zaidi ya mchezaji anayemfuata na ametaja hadharani kuchanganyikiwa kwake juu ya hali hiyo.

PSG ilitajwa kama mahali pazuri pa kutua Salah iwapo ataondoka Liverpool, ingawa Al-Khelaifi tayari amezima habari zinazodai kuwa ana nia ya kutaka kumnunua mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32.

Wakati akihudhuria droo ya Kombe la klabu bingwa ya Dunia rais huyo wa PSG aliiambia GIVEMESPORT: "Nampenda Salah, pia kwa sababu alitoka sehemu yetu ya dunia. Ninajivunia sana, kusema ukweli, kwa kile alichokifanya katika Ligi Kuu ya England akiwa na Liverpool.

"Na nina heshima kubwa kwake na kwa Liverpool. Kwa hivyo hatukuwahi kuzungumza naye. Naiheshimu Liverpool, namuheshimu mchezaji, ana mkataba na Liverpool na hatukuwahi kuzungumza naye."

Kocha wa Liverpool, Arne Slot tayari amekiri ni "ngumu kutabiri" ikiwa Salah atasalia Merseyside zaidi ya msimu huu.

Liverpool wako katika nafasi nzuri kwenye Ligi Kuu na Ligi ya Mabingwa lakini wana matatizo mengine ya mikataba huku nyota wengine Virgil van Dijk na Trent Alexander-Arnold pia wakiwa na mikataba ambayo inaisha msimu wa majira ya joto.

# RONALDO MAMBO MAGUMU AL NASSR




**JEDDAH,** Saudi Arabia

CRISTIANO Ronaldo na Karim Benzema kila mnoja aliifungia bao timu yake katika mpambano wa Al Ittihad dhidi ya Al Nassr kwenye ligi Kuu Saudia Ijumaa, lakini ni timu ya fowadi wa Ufaransa iliyopata bao la dakika za mwisho la ushindi na kuimarisha matumaini yao ya ubingwa.

Ushindi wa Al Ittihad wa 2-1 wa tisa mfululizo katika Uwanja wa King Abdullah Sports City huko Jeddah uliwafanya wasogee kileleni kwa pointi tano, kabla ya Al Hilal iliyo nafasi ya pili kucheza jana Jumamosi.

Bao la Benzema dakika ya 55 likiwa ni la 10 katika mechi 10 za ligi -liliwapa wenyeji bao la kuongoza kabla ya Ronaldo kupiga shuti lililompita Predrag Rajkovic dakika mbili baadaye na kusawazisha.

Mshambuliaji wa zamani wa Tottenham Hotspur, Steven Bergwign aliipatia Al Ittihad pointi zote tatu kwa shuti kali kutoka pembeni ya eneo la goli lililoingia kwenye kona ya mbali katika kipindi cha pili.

Al Nassr watamenyana na Al Akhdoud katika mechi yao inayofuata Januari 9, huku Al Ittihad wakimenyana na Al Hilal ya Neymar katika robo fainali ya Kombe la Mfalme Januari 7.

# Amorim: Manchester Utd ni klabu kubwa, si timu kubwa



**MANCHESTER,** England

RUBEN Amorim amesema amerithi nafasi ngumu Manchester United na akaelezea timu yake mpya kama "klabu kubwa lakini si timu kubwa."

Baada ya kunyakua mataji 20 ya Ligi Kuu, United ndio klabu yenye mafanikio zaidi katika soka la England.

Lakini historia yao ya kuvutia imeathiriwa na matokeo mabaya ya uwanjani katika muongo mmoja uliopita.

Amorim amewasili United, ambao hawajashinda taji tangu mwaka 2013.

"Sisi ni klabu kubwa lakini sisi sio timu kubwa," alisema Amorim akiwaambia waandishi wa habari.

"Wachezaji wetu wanapaswa kuelewa kwamba ni nafasi ngumu sana.

"Sisi sio moja ya timu bora kwenye ligi na tunapaswa kusema na kufikiria hilo waziwazi, lakini ubora wetu haupo tena kwenye ligi.

"Kwa hiyo hapa tuna tatizo na tunapaswa kuzingatia mambo madogo na maelezo madogo."

Amorim amekuwa na muda mchache kwenye uwanja wa mazoezi tangu achukue mikoba kutoka kwa Erik ten Hag kwa sababu ya orodha ya wachezaji.

Kocha huyo mwenye umri wa miaka 39 amekuwa mwangalifu kupunguza matarajio yake wakati kikosi kikikabiliwa na mpangilio mpya wa kimbinu.

Hata hivyo, anasisitiza jambo lisiloweza kujadiliwa ni kiasi cha juhudi zinazowekwa na wachezaji wake na kuwaonya kuwa wanapaswa "kukimbia kama mbwa wenye wazimu" ikiwa wanataka kufanikiwa.

"Nadhani jinsi tunavyorudi nyuma, jinsi tunavyokimbia mbele, jinsi tunavyopigana, tunapaswa kuwa wazi na timu, hii ni hatua ya kwanza tunapaswa kushughulikia kisha masuala ya kimbinu na kiufundi yanakuja baadaye," aliongeza Amorim.

# Pulisic azua hofu Milan

**MILAN,** Italia

NAHODHA wa timu ya taifa ya Marekani, Christian Pulisic alilazimika kutoka nje ya uwanja kutokana na jeraha la mguu wa kulia wakati wa kipindi cha kwanza huku AC Milan ikichapwa 2-1 na Atalanta, Ijumaa.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 nafasi yake ilichukuliwa na Ruben Loftus-Cheek dakika ya 38 ya mechi kwenye Uwanja wa Gewiss wa Atalanta baada ya kuonekana kuteleza baadae ya kuchezewa vibaya na Mario Pasalic.

Mmarekani huyo, ambaye shuti lake lililookolewa mapema kwenye mechi hiyo, alikaa chini kwa maumivu, akishika kifundo cha mguu.

Licha ya kujaribu kucheza huku akiwa na maumivu, alitoa ishara kwa benchi kwamba alihitaji kutoka.

Kisha Pulisic alisaidiwa kutoka nje ya uwanja. Baada ya mechi, kocha wa Milan, Paulo Fonseca alitoa taarifa ya kutia moyo kuhusu jeraha la Pulisic.

"Ni shida ndogo, hakuna kitu kikubwa," alisema katika mkutano wake na wanahabari baada ya mchezo.

Katika msimu wake wa pili akiwa na Milan, Pulisic amefunga mabao nane na kutoa asisti sita katika mechi 19. Jeraha la Pulisic ni wasiwasi kwa klabu yake kabla ya mechi muhimu ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Red Star Belgrade siku ya Jumatano.

Ademola Lookman alifungia Atalanta bao la ushindi la dakika za lala salama ambalo liliwapeleka wenyeji kileleni mwa Serie A na kurefusha mfululizo wao wa ushindi hadi michezo tisa katika mashindano yote.

Fonseca pia alimshutumu mwamuzi Federico La Penna kwa kutoonyesha heshima ya kutosha kwa upande wake baada ya kuchapwa na Atalanta.

"Siogopi kusema ukweli. Siku zote niliheshimu kazi ya waamuzi, natambua wana kazi ngumu, lakini kila wiki huwa ni sawa," Fonseca aliiambia Sky Sport Italia.

"Jinsi mwamuzi alivyochezesha jioni hii ilikuwa ni ukosefu wa heshima kwa Milan."



## Simba kamili

INATOKA UK. 24

tatu muhimu katika mchezo wa leo. Wachezaji hao ni kiungo mshambuliaji, Abdennour Iheb Belhocini mwenye mabao mawili na asisti' moja katika michezo 10, kiungo mkabaji Salifou Tapsoba aliyetumika katika michezo sita ya timu hiyo na straika, Mounder Temine.

"Tamine na Belhoussini hatutakuwa nao kutokana na majeraha, Tapsoba ameondoka kwa ajili ya majukumu ya kimataifa, tunapokosa wachezaji muhimu tunajua kuwa tutakutana na changamoto kubwa. Hii ni hali inayotufanya tuwe na wasiwasi," alisema Madoui

Hata hivyo, alisema anatarajia wachezaji waliopo watapambana kwa nguvu kuhakikisha wanapata matokeo mazuri.

"Simba ni timu inayoheshimiwa sana katika mashindano ya kimataifa kutokana na uzoefu wake, tunahitaji kujiandaa kwa umakini, tunajua kuwa mchezo huu ni muhimu sana kwetu kwa sababu pointi zake zitakuwa na maana kubwa katika safari yetu ya kufika mbali katika michuano hii," alisema kocha huyo.

## Yanga SC pointi nyingi ugenini...

INATOKA UK. 24

bao mengi ikicheza uwanja wake wa nyumbani.

Simba imepachika mabao 16, kati ya 22 ambayo imeyafunga mpaka sasa, ikicheza nyumbani ambapo imeshuka dimbani mara sita, ikishinda nne, sare moja na kupoteza mchezo mmoja dhidi ya Yanga.

Timu ya Fountain Gate inafuatia kwa kupachika mabao mengi ikiwa nyumbani, ikifanya hivyo mara 12, kati ya 20 iliyofunga kwenye Ligi Kuu mpaka sasa.

Timu hiyo inafuatiwa na Yanga pamoja na Azam zinashika nafasi ya tatu ambazo zote zimepachika mabao manane kila moja ikicheza viwanja vya nyumbani.

Timu za JKT Tanzania, Dodoma Jiji, Singida Black Stars, na Coastal Union zipo kwenye nafasi ya nne kwa kufunga mabao mengi nyumbani, zikifunga mabao saba mpaka sasa.

# JKT TANZANIA YATOA ONYO KOMBE LA FA

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya JKT Tanzania imekuwa timu pekee iliyopata ushindi mkubwa zaidi katika mechi za raundi ya tatu ya Kombe la Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), maarufu Kombe la FA katika mechi sita zilizopigwa juzi kwenye viwanja mbalimbali ikiikandamiza Igunga FC mabao 5-1.

Baada ya ushindi huo, Ofisa Habari wa klabu hiyo, Masau Bwire alisema hilo ni onyo kwa timu zingine zinazoshiriki michuano hiyo.

**Masau amesema msimu huu wamedhamiria kufanya vyema kweli Ligi Kuu na Kombe la Shirikisho hivyo kuzitahadharisha timu itakazopangwa nazo kwenye Kombe la FA kutarajia kipigo kama hicho.**

"Ni kipigo tulichotarajia kuwapiga, kwa sasa hatuna shaka, timu yoyote itakayopata bahati mbaya ya kukutana na sisi itarajie kuwakuta kilichowakuta Igunga FC," alisema Masau.

JKT Tanzania ilikuwa kwenye uwanja wake wa nyumbani, Meja Jenerali Isamuhyo, Mbweni, Dar es Salaam, ikipata ushindi huo na kufanikiwa kutinga hatua ya 16 bora.

Nahodha wa kikosi hicho, John Bocco aliwaongoza vyema wenzake, akiwa mmoja wa waliofunga mabao hayo, dakika ya 14, likiwa ni bao la pili kwenye mchezo huo, likitanguliwa na bao la Wilson Nangu dakika ya 12, Mohamed Bakari, akifunga mabao mawili, dakika ya 16 na 30, huku Dany Lyanga akipigilia msumari wa mwisho kwenye jeneza la wageni wao kutoka Tabora.

Timu zingine zilizopata ushindi na kutinga hatua hiyo, ni Cosmopolitan iliyoichapa Nyota Academy mabao 2-0, Stand United nayo ikapata ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Don Bosco, Polisi Tanzania ilipata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Bukombe Combine huku, Namungo nayo ikipata ushindi nyumbani wa mabao 2-0 dhidi ya Tanesco FC.



Mdhamini wa pambano la ngumi la 'Fight for Change', Abdulrahim Noray (kulia) akikabidhi msaada kwa mlezi wa kituo cha Malaika, Neema Mohamed, jana jijini Dar es Salaam, kulia ni bondia Karim Bhaloo. **PICHA: FAUSTINE FELICIANE**

# *Bondia, mdhamini watoa msaada watoto yatima*

**Na Faustine Feliciane**

BAADA ya kufanyika kwa pambano la ngumi la 'Fight for Change' wiki iliyopita waandaaji wametimiza ahadi kwa kutoa msaada kwa kituo cha kulelea watoto yatima na wanaoishi katika mazingira magumu cha Malaika, jijini Dar es Salaam.

Akizungumza wakati wa kukabidhi msaada huo, muandaaji wa pambano hilo ambaye pia ni bondia, Karim Bhaloo, amesema wametimiza ahadi waliyoitoa kabla ya pambano hilo kwa kutoa msaada huo.

"'Figt for Change' ina lenga kusaidia zaidi jamii, tulipanga kutoa msaada huu na leo tumetimiza, tutakuwa tukifanya hivi kila tunapoandaa pambano," alisema Bhaloo.

Alisema msaada walioutoa ni pamoja na vyakula, mafuta ya kupika, sabuni, sukari, mitungi ya gesi na bidhaa nyinginezo.

Aidha, mmoja wadhamini wa pambano hilo, Abdulrahim Noray ambaye ni mkurugenzi w akampuni ya Oscon Builders, alisema wataendelea kudhamini kuunga mkono juhudi za waandaji wapambano hilo katika kusaidia jamii.

"Nifahari kwetu kuona wanamichezo wanakumbuka jamii, msaada huu ni chachu kwa mabondia na wanamichezo wengine kuwasaidia watanzania wenzetu pale wanapopata nafasi kama walivyofanya hawa wenzetu," alisema Noray.

Kwa upande wake, mlezi wa kituo hicho, Neema Mohamed, alishukuru kwa msaada huo na kutoa wito kwa watu wengine kuwasaidia kwa kuwa watoto wanaolelewa katika kituo hicho wana uhitaji mkubwa.

"Kituo hiki cha Kinondoni kuna watoto 32 ambao wapo wanafunzi kuanzia chekechea mpaka wengine ngazi ya vyuo, uhitaji ni mkubwa sana kwenye eneo la elimu na afya, tuwaombe watanzania wenzetu kuendelea kutusaidia," alisema Neema.

# Michezo

Jumapili Desemba 8, 2024

Nipashe



Ronaldo mambo magumu Al Nassr UKURASA 22



Mabeki wa Simba, Shomari Kapombe (kushoto) na Che Malone wakiwa kwenye mazoezi ya timu hiyo jana kwenye mji wa Costantine, Algeria. **PICHA: SIMBA SC**

# Simba kamili kuivaa CS Constantine FC

**Na Mwandishi Wetu**

●●● Kocha Fadlu anasa faili la wapinzani wao hao, atamba kila kitu kwa sasa....

KIKOSI cha Simba leo saa 1:00 usiku kwa saa za Tanzania, kitashuka kwenye Uwanja wa Mohamed Hamlaoui kwenye mji wa Constantine nchini Algeria, kucheza dhidi ya CS Constantine katika mchezo wa raundi ya pili Kombe la Shirikisho Afrika hatua ya makundi, huku Kocha Mkuu wa timu hiyo, Fadlu Davids, amesema watacheza mchezo huo kimkakati, huku wapinzani wao wakilia kuwakosa wachezaji watatu muhimu.

Katika mchezo huo wa Kundi A, timu zote zitaingia uwanjani zikiwa na kumbukumbu ya kushinda mechi zao za raundi ya kwanza, Simba ikishinda nyumbani bao 1-0 dhidi ya Bravo do Maquis ya Angola na CS Constantine ikishinda bao 1-0 dhidi ya CS Sfaxien ya Tunisia.

**Timu yoyote itakayoshinda mchezo wa leo itakaa juu ya kilele cha msimamo wa kundi hilo.**

Kocha Fadlu amesema maandalizi ya mchezo huo yamekamilika, ikiwemo kuwasoma wapinzani wake, jinsi wanavyocheza na wachezaji wao bora na hatari na amewaelekeza wachezaji wake jinsi gani ya kukabiliana nao.

"Mandalizi yamekamilika, nimefurahi kuja kwa golikipa Hussein Abel ili kuongeza idadi yao kama lolote likitokea, natarajia mechi itakuwa ngumu na ya kasi sana, tumejiandaa kwa hilo, nimewaona wana mabeki wazuri, lakini katika mchezo huu ni muhimu kwetu kupata bao ili kutuweka mchezoni," alisema.

Fadlu, raia wa Afrika Kusini, alisema katika mechi ya leo, wachezaji wake wanatakiwa kuwa na kasi wakati wanashambulia, lakini wanaponyang'anywa mpira amewaelekeza kuwa na nidhamu ya kurudi nyuma haraka ili kusaidia ulinzi.

"Tunatakiwa kucheza mechi hii kimkakati, siyo ili mradi tunacheza, kwa sababu tuna machaguo mawili, kushinda au kutoa sare, hivyo hatutakiwi kufunguka sana, ila tunapokuwa na mpira tunatakiwa tuwe na kasi na maamuzi ya haraka," alisema Fadlu.

Kocha Mkuu wa CS Constantine, Kheireddine Madoui, ameonekana kuhuzunika kuwakosa wachezaji wake wa

INAENDELEA UK. 23

## Yanga pointi nyingi ugenini, Simba mabao mengi nyumbani

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI zikiwa zimesimama kwa muda kucheza mechi za Ligi Kuu wiki hii kutokana na kuwa na majukumu ya mechi za kimataifa, Mabingwa Watetezi Yanga wameonekana kuvuna pointi nyingi ikicheza ugenini, huku Simba ikipachika mabao mengi ikicheza nyumbani.

Kwa mujibu wa takwimu za dawati la michezo la gazeti hili, Yanga pamoja na kushika nafasi ya tatu kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, ikiwa na pointi 27, inaongoza kwa kuzoa pointi nyingi ugenini, ikiwa imekusanya pointi 18.

Timu hiyo imekusanya pointi tisa tu ikicheza kwenye uwanja wake wa nyumbani.

Yanga imecheza michezo sita ikiwa ugenini, ikishinda yote, ikifunga mabao manane, na kutoruhusu bao lolote.

Imecheza michezo mitano nyumbani, ikishinda mitatu na kupoteza miwili, ikifunga mabao manane na kuruhusu manne.

Yanga inafuatiwa na Azam FC, ambayo imekusanya pointi 17 ikicheza ugenini, imecheza mechi saba, imeshinda michezo mitano, sare mbili na haijapoteza mechi yoyote.

Katika michezo yake ya nyumbani, Azam, imeshuka dimbani mara sita, ikishinda mara nne, sare moja na kupoteza mmoja mbele ya Simba kwa mabao 2-0, mechi ikichezwa, Uwanja wa New Amaan Zanzibar, Septemba 26, ambapo Wanalambalamba waliutumia kama uwanja wao wa nyumbani.

Simba inashika nafasi ya tatu ikizoa pointi 15 ugenini, Singida Black Stars ni ya nne ikiwa imekusanya pointi 13.

Wakati hayo yakiendelea, timu ya Simba inaongoza kwenye Ligi Kuu kwa kufunga ma-

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >